EAST AFRICANA COLLECTION



MADA: Katama Mkangi: Mwandishi chipukizi anayeng'ang'ania nafasi katika uwanja wa fasihi?

Beja, S. Karisa

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa kwa minajili ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya 'Bachelor of Arts' katika Chuo Kikuu cha Nairobi Mwaka wa 1986.

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

## IKIRARI

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada ya digrii yoyote katika Chuo Kikuu chengine chochote"

S. Karisa Beja

(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii".

..........................

Dkt. Jay Kitsao

..........................

Bw. E. Kazungu

# YALIYOMO

SURA YA KWANZA UKURASA

1.0 Utangulizi.................... 1

1.1 Jambo la kushughulikia....... 2

1.2 Madhumuni ya tasnifu hii..... 4

1.3 Upeo wa tasnifu.............. 6

1.4 Sababu za kuchagua mada hii.. 6

1.5 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili. 7

1.6 Msingi wa nadharia wa tasnifu hii................... 8

1.7 Njia za utafiti............... 12

Tanbihi...................... 14

SURA YA PILI

2.0 Utangulizi.................... 16

1.1.1 Ukiwa........................ 18

2.1.2 Mafuta....................... 21

2.2 UJENZI WA RIWAYA.............. 25

Mfulilizo wa hadithi.......... 26

Mtindo wa Usimulizi........... 28

Matumizi ya lugha............. 37

Uchoraji wa wahusika.......... 45

2.3 UTEUZI WA MAUDHUI............ 49

Maudhui...................... 49

Mafunzo...................... 55

Misimamo na falsafa za mwandishi...................... 59

HITIMISHO...................... 62

2.4 UYAKINIFU WA MKANGI KATIKA RIWAYA ZAKE......................... 63

2.5 Hitimisho...................... 65

Tanbihi.........................

MAREJELEO....................

## SHUKRANI

Ni vigumu kuwataja majina watu wote walionisaidia na mawaidha yao katika kazi hii. Hata hivyo sina budi kuwataja na kuwashukuru sana Dr. Jay Kitsao na Mr. E. Kazungu kwa kuusoma mara kwa mara mswaada wa tasnifu hii na kunipa mashauri yao ya busara hasa katika mahali waliponi-ona naenda kombo.

Aidha ninawashukuru Bw. Lazarus Mwachinda, Bw. Kahindi Zia, Bw. B.S.M. Sirucha na Bw. B.M. Kanga kwa mawaidha waliyonipatia mara kwa mara katika mazungumzo yetu kuhusu tasnifu hii. Pia sitasahau kuwashukuru wanafunzi wa Kiswahili wa mwaka wa tatu hasa wale waliowahi kunichotea baadhi ya masaa yao muhimu ili nizungumze nao kuhusu maoni yao na misimamo yao juu ya Mkangi kama mwandishi wa fasihi riwaya.

Hasahauliki Bi. Jane Mutharia kwa kupiga chapa tasnifu hii kwa moyo mkunjufu na kwa bidii.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Wataalamu wengi wa fasihi wanakubaliana kwamba fasihi ni kioo kinachomulika hali halisi ya maisha ya jamii kwa njia ya kubuni na kutumia lugha kisanaa. Kwa mujibu wa fasili hii fasihi - ikiwa na tanzu zake tatu: riwaya, ushairi na tamthilia - ni zao la jamii. Kwa hivyo twaweza kusema ya kwamba maisha ya jamii ndiyo migodi ya malighafi ya fasihi na sanaa kwa jumla. Kawaida maisha ya jamii huwa yanaathiriwa sana na hali ya uchumi, siasa na historia ya jamii hiyo. Kwa hivyo fasihi pia ina jukumu muhimu la kutuchorea ukweli halisi wa maisha ya jamii na kiini cha hali hiyo ya maisha na kujaribu kupendekeza namna ya kutatua madhila hayo. Kufuatana na maelezo haya ya fasihi na jukumu lake, kila mtunzi anawajibika kuchota taarifa yake kutoka katika jamii na kuibusha falsafa zake za maisha ya binadamu kulingana na tajriba ya maisha yake. Kwa muktadha huu, katika tasnifu hii tutazichambua na kuzichanganua riwaya mbili - Ukiwa na Mafuta za Katama Mkangi alizowahi kuandika na kuzichapisha hadi wakati wa kuandika tasnifu hii. Tutafanya hivyo kwa madhumuni ya kumwangalia Mkangi kama mwandishi chipukizi wa fasihi riwaya.

Tutaangalia maudhui na ujenzi wa riwaya zake kwa jumla. Tutatizama Ukiwa kwanza halafu Mafuta ili tuweze kuumulika na kuufuata ukuaji wa tajriba na mawazo ya mwandishi huyu pamoja na mabadiliko kwa jumla ya ujuzi na uwezo wa uandishi wake wa riwaya katika uwanja wa fasihi.

## 1.1. JAMBO LA KUSHUGHULIKIA

Mada ya tasnifu hii ni: Katama Mkangi kama mwandishi chipukizi katika uwanja wa fasihi. Kuambatana na mada hii nitashughulikia katika tasnifu hii, kumwangalia Katama Mkangi kama mwandishi - msomi na msanii anayeng'ang'ania nafasi katika uwanja wa fasihi riwaya za Kiswahili. Aghlabu mwandishi akijitosa katika utunzi na kuanza kupata sifa basi huingiwa na ilhamu ya kuandika zaidi. Huanza kujizatiti na kutunga na kuandika zaidi na zaidi pengine hadi kufikia kilele cha uwezo wake. Hufanya hivyo kwa madhumuni ya kuendelea kuwafunulia wasomaji ukweli wa hali halisi ya baadhi ya vipengee vya maisha. Aidha anapoendelea kuandika huwa pia anajenga jina lake kama mtunzi katika uwanja wa fasihi. Sana, kama inavyoelekea, mtunzi hushikilia utanzu fulani wa fasihi kama vile riwaya au ushairi ama tamthilia. Kisha huendelea kujikuza na kujijenga katika

utanzu huu kama tunavyowaona wandishi wengine kama Jay Kitsao[1] na E. Hussein[2] walioshikilia utanzu wa tamthilia. Kuna pia E. Kezilahabi[3] na S.A. Mohamed[4] walioegemea sana katika riwaya kuliko katika ushairi. Hata hivyo wako wengine walioweza kujijenga vilivyo katika zaidi ya utanzu mmoja wa fasihi kama vile Shaaban Robert[5] aliyewahi kuegemea katika riwaya na ushairi.

Nitashughulikia pia kumwangalia Mkangi katika uyakinifu wa kazi zake. Hii ni kwa sababu fasihi kama nilivyotangulia kusema ina jukumu na kazi maalumu katika jamii kama D. Lucas anavyosisitiza:-

> "Kila kazi ya fasihi kupitia yaliyomo, mtindo wake wa lugha, taswira, mdundo nk. lazima izushe mioyoni mwetu uhusiano wa mawazo na hisia, na kuzusha matendo na fikira zinazoweza kutukusanya dhidi ya au kupendelea jambo fulani"[6]
>
> (Tafsiri ni yangu)

Kwa mujibu wa dondoo hii mwandishi hutunga na kuandika riwaya yake akiwa na madhumuni kama ya kufurahisha au kuasa, kuelimisha au kujulisha umma mambo yaliyompitikia katika tajriba ya maisha yake. Kwa

hivyo tutashughulikia kuangalia ukamilifu, ukweli na mlengo wa hadithi za Mkangi kulingana na hali halisi ya maisha ya jamii anayoizungumzia.

Fauka ya hayo nitashughulikia kuangalia ufūndi wa Mkangi katika uteuzi wa maudhui, uchoraji wa wahusika, usimulizi wa hadithi na matumizi ya lugha na jinsi alivyovitumia vipengee hivi vyote katika kuzijenga riwaya zake kwa jumla.

## 1.2. MADHUMUNI YA TASNIFU HII

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

Madhumuni ya tasnifu hii ni kumulika aina ya maudhui Mkangi anayojishughulisha nayo katika Ukiwa na Mafuta. Jambo hili litatuonyesha kiasi cha uzingatifu wa mwandishi huyu juu ya hali na maslahi ya jamii na historia yake katika kazi zake hizi za fasihi, pamoja na msimamo wake kuhusu mapenzi, utamaduni na siasa.

Aidha tasnifu hii ina madhumuni ya kudhihirisha kiasi cha kipawa cha mwandishi pamoja na kiasi cha uzito wa mawazo na umahiri wake katika utunzi na uandishi wa fasihi riwaya. Mambo haya yote yatatusaidia kuamua ikiwa nafasi anayoing'ang'ania Mkangi katika uwanja wa fasihi anaipata au inambidi akaze mshipi wake katika utunzi. Mwandishi hupata nafasi katika uwanja wa fasihi kwa sifa na shime

anazopata kutoka kwa jamii hasa wasomaji wake. Hupata sifa sio kulingana na idadi na mchango wa kazi zake katika fasihi tu bali na umbuji wa utunzi anaowaandalia wasomaji wake hasa katika uteuzi wa maudhui akizingatia maisha halisi ya jamii na maslahi yao, matumizi ya lugha kisanaa na mjengo wa riwaya zake kwa jumla. Tena huwa kazi zake za fasihi zinapendwa na kufurahikiwa na wengi. Baadhi ya watunzi waliomtangulia Mkangi na kuhesabika kuwa wamepata nafasi katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili ni marehemu Shaaban Robert mwenye upevu wa uandishi ambaye anajulikana kama "Baba wa riwaya" Pia kuna M.S. Abdalla mwandishi anayejulikana katika uwanja wa riwaya za upelelezi; S.A. Mohamed ajulikana kama mwandishi mashuhuri tena msomi anayepinga ubwanyenye na ukabaila.

Kuna dhana ya uandishi inayosema "Jinsi mwandishi aendeleavyo kuandika ndivyo akuavyo katika fani hiyo ya uandishi"[7] Kuambatana na dhana hii tasnifu hii ina madhumuni pia ya kudhihirisha ufundi wa mwandishi kutoka kazi yake ya kwanza ya fasihi riwaya - Ukiwa na kazi yake ya pili - Mafuta ili tuweze kuamua ikiwa dhana hii inalingana na Mkangi ama yuko kinyume chake.

## 1.3. UPEO WA TASNIFU

Katika kumwangalia Mkangi kama mwandishi chipukizi nitajifunga na kazi zake mbili tu za Ukiwa na Mafuta ambazo nimezisoma na kuzitalii hadi wakati wa kuandika tasnifu hii. Kwa hivyo tasnifu hii haitajishughulisha na kazi yoyote ya fasihi ya Mkangi ambayo haijachapishwa na kutolewa kwa wakati huu.

Katika kumwangalia mwandishi huyu nitajikita zaidi katika maudhui na ujenzi wa riwaya zake kwa jumla. Kwa ufupi uchanganuzi wa riwaya hizi za Mkangi utakuwa wa kifasihi ambapo nitajishughusha na kuangalia dhamira, maudhui na mitindo anayoitumia katika kuwasilisha ujumbe wake.

## 1.4. SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Kwanza, hakuna mpaka sasa mtu yeyote aliyemwangalia Katama Mkangi kama mwandishi - msomi na msanii wa fasihi riwaya kwa utaratibu na mtindo ninaoufuata mimi.

Pili, Mkangi ni mwandishi wa kisasa ambaye ameandika mpaka sasa riwaya mbili. Fauka ya hayo ni mmoja wa waandishi wachache sana nchini ambao tunaweza kuwataja kwa juhudi zao za kujishughulisha na utunzi wa fasihi riwaya. Hivi sasa riwaya zake

hizi Ukiwa na Mafuta zinaanza kupata umaarufu kwa kutumiwa kama vitabu vya mtihani katika shule na vyuo vikuu humu Kenya. Jambo hili pia limenipa ari ya kumwangalia mwandishi huyu na kuangaza angaza yaliyomo katika riwaya hizi.

## 1.5 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Machache yameandikwa kuhusu Mkangi kama mwandishi. Yuko Kivutha Kibwana ambaye ametoa kwa muhtasari tu mawazo yake katika gazeti la kila wiki la 'The weekly Review'[8] juu ya riwaya ya Mafuta kama mapitio tu. Katika mapitio haya Kibwana ametoa muhtasari wa hadithi ya Mafuta na kugusia kuwa Mafuta imeandikwa kwa kiswahili chepesi kama Ukiwa na kwamba anapendezwa na utumiaji wake wa jazanda, na wazo la kujenga hadithi ya Mafuta katika nchi ya kubuni ijapo inaweza kusemekana inahusu nchi zinazoendelea. Anamalizia na kumsifu Mkangi kwa mchango wake katika fasihi ya Kiswahili kama walivyofanya kina E. Hussein, Abdilalif Abdalla na S.A. Mohamed.

Jay Kitsao naye katika tasnifu yake ya Ph.D aliangalia Ukiwa kama moja ya riwaya alizozishughulikia. Jay Kitsao alijikita katika muundo na ujenzi wa sentensi za riwaya ya Ukiwa baada ya kutoa muhtasari wa hadithi ya riwaya yenyewe.

Pia yuko Daniel Katuu ambaye katika kitabu chake cha Uchambuzi wa Vitabu Vya Kiswahili amefanya uchambuzi wa Ukiwa wa kiwango cha kidato cha nne ambapo kwanza ametoa mawazo yaliyomo katika Ukiwa kama vile migongano ya fikira inayotokana na nyendo na tabia zilizoathiriwa na uzungu, na kwamba mapenzi ya uaminifu ndio mwanzo wa ndoa. Pia Katuu amegusia kwamba Ukiwa ni kumbukumbu kwa Matano. Kisha akamsifu mwandishi kuwa ameeleza kila kitu kwa undani hasa kuhusu mapenzi na uhusiano wa Matano na Lila. Baadaye anatoa muhtasari wa hadithi hii ya Ukiwa.

## 1.6 MSINGI WA NADHARIA WA TASNIFU HII

Iko misingi mingi ya nadharia ambayo hutumiwa na wachambuzi na wahakiki wa kazi za fasihi na sanaa kwa jumla. Utumiaji wa misingi ya nadharia fulani hutegemea sana madhumuni ya mhakiki wa kazi hiyo ya fasihi. Baadhi ya nadharia zenye misingi inayotumika katika fasihi ni:-

1) Nadharia inayozingatia muundo wa kazi ya sanaa. Kwa kiingereza nadharia hii huitwa "Structuralism". Nadharia hii huwa haijishughulishi na yaliyomo katika fasihi na sanaa kwa jumla bali hujishughulisha na jinsi sanaa hiyo ilivyoumbika.

2) Pia iko nadharia inayozingatia sana namna mwandishi anavyoeleza kuliko muundo wa fasihi katika kazi yoyote ya fasihi. Nadharia hii huitwa kwa kiingereza "Expressionism".

3) Kisha kuna nadharia ya Ki Marx-Kilenin ambayo ina sifa za uzingatiifu wa uzito wa mawazo ya jambo lililoandikwa pamoja na usanii wa msanii.

Kwa sababu tasnifu hii itajishughulisha na kumwangalia Mkangi kama mwandishi wa fasihi riwaya hatuna budi kuchambua na kuchanganua kazi zake kifasihi. Kwa hivyo ni mwafaka mno tukitumia msingi wa nadharia ya ki Marx-kiLenin kwani ndiyo itakayotuongoza vyema katika kumulika kwa undani uzito wa aliyoyaandika mwandishi huyu pamoja na ufundi wake. Hii ni kwa sababu nadharia hii inasisitiza zaidi uhusiano wa sanaa na jamii na kushikilia kwamba fasihi ni zao la jamii.

Nadharia hii pia ina misingi yake iliyojikita katika uhusiano wa kisiasa na kiuchumi kama dhana muhimu zinazounda mazingira ya jamii kulingana na misimu ya kihistoria. Mbali na kujishughulisha na yaliyomo na muundo katika fasihi nadharia hii

inahimiza umuhimu wa mtindo katika fasihi kama chombo cha kuendeleza maudhui. Fauka ya hayo, nadharia hii ya Ki Marx inashikilia na kuhimiza kuwa fasihi ni ile inayojitambulisha na matazamio na maslahi ya walio wengi katika wakati fulani wa historia. Kwa hivyo fasihi ya namna hii ni lazima ijishughulishe kwa kiwango fulani na siasa. Hivyo basi mwandishi huandika, kama H. Arvon[9] alivyosema baada ya kutoweza kuhimili msukumo anaopata moyoni mwake kuhusu mapambano ya kitabaka anayoyaona katika jamii na alazimike kujitambulisha na tabaka moja, lile la walio wengi. Mao Tse Tung naye aliongeza kusema:

> "Kazi kubwa ya mwandishi na msanii ni kudhihirisha unyama na uonevu wa mabwanyenye kwa wadhulumiwa katika harakati za kujikomboa ili kuwapa nguvu makabwela wajue kwamba unyama wauonyeshwao waweza kuondolewa (Tafsiri ni yangu)"[10]

Kwa jumla nadharia hii ya ki Marx ni nadharia ambayo inapinga kinagaubaga ile ibara ya "sanaa kwa minajili ya sanaa,"[11] inayoshikilia kwamba jamii iko kwa madhumuni ya sanaa wala si kwamba sanaa iko kwa madhumuni ya jamii. Kauli hii inaonyesha kuwa

ibara hii vilevile inashikilia kuwa sanaa ni umbo - yaani vile ilivyojengeka kimuundo. Lakini falsafa za ki Marx zashikilia kuwa sanaa imo katika umbo la kazi hiyo ya sanaa na katika uzito wa mawazo yaliyomo katika sanaa hiyo. Kwa muktadha huu umbo la sanaa linawajibika kurembwa na baadhi ya mambo haya:-

1) Kudhihirisha kiini cha mapambano halisi ya jamii dhidi ya mazingira yanayomdhalilisha binadamu na kumnyima ubinadamu katika harakati zake za maisha. Kwa hivyo fasihi ni idhihirishe "mapenzi ya ubinadamu".

2) Kudhihirisha mwamko wa kisiasa wa mawazo ya upinzani yaliyoko kati ya mabwanyenye na makabwela.

3) Sanaa iweze kuzusha hisia na ilenge kudhihirisha hali halisi ya maisha katika jamii anayozungumzia msanii na kujaribu kuiumba hali hiyo.

4) Sanaa ni imwezeshe msomaji kuiona dunia ya matatizo anayoishi na aweze kuwa sio msomaji tu bali mshiriki wa hali hiyo wa mwenye moyo na ari ya kubatilisha hali hiyo. Ama aweze kujirudi pale astahilipo.

Matakwa haya yote ya fasihi kulingana na misingi ya nadharia ya ki Marx yanaeleza kwa nini falsafa za ki Marx hutumika sana kuchunguza athari za uchumi na siasa katika jamii kwa wakati fulani wa kihistoria ikisisitiza umuhimu wa mabadiliko katika mfumo wa jamii na hali ya binadamu kwa jumla. Hii ndiyo sababu kwa nini hivi leo waandishi wengi hutunga kazi za fasihi zinazoambatana na jukumu fulani la kisiasa ama kijamii. Kwa hivyo misingi ya nadharia ya ki Marx - kiLenin itatufaa sana katika kumwangalia Mkangi kama mwandishi wa fasihi riwaya. Hii ni kwa sababu nadharia hii inapendekeza kuwa mtunzi yeyote ni adhihirishe waziwazi hali halisi na maslahi ya jamii ya wakati wake tena kwa ubora zaidi kuliko waandishi wengine.

## 1.7 NJIA ZA UTAFITI

Madhumuni ya sehemu hii ni kudokezea njia nilizofuata na kunisaidia kumwangalia Mkangi kwa namna nilivyomwangalia katika tasnifu hii.

Nimesoma na kuzichambua riwaya mbili hizi za Mkangi - Ukiwa - Mafuta - kwa madhumuni ya kuzitalii na kuniwezesha kumuelewa na kumwangalia mwandishi huyu kifasihi.

Nimesoma makala kuhusu ujenzi wa sentence (muundo) katika Ukiwa yaliyoandikwa na Jay Kitsao

katika tasnifu yake ya Ph.D. Pia nimesoma mapitio ya kitabu cha Mafuta yaliyoandikwa na Kivutha Kibwana katika gazeti la kila wiki la "The Weekly Review" toleo la Septemba 20, mwaka wa 1985.

Kadhalika nimesoma pia kitabu cha D. Katuu kiitwacho Uchambuzi wa Vitabu vya Kiswahili. Katika kitabu hiki nimesoma sehemu inayochambua kijuu juu tu riwaya ya Ukiwa.

Aidha nimesoma vitabu katika maktaba kuhusu nadharia na falsafa za ki Marx - kiLenin na fasihi. Baadhi ya vitabu hivyo ni:-
Marxism and Art, B. Lang & F. Williams; Art and Society, Sanchez, V.A.; na The Structure of Literary Understanding, Olsen, S.A.

Nimewahi kumhoji Mkangi mwandishi wa riwaya hizi mbili - Ukiwa na Mafuta. Nimechuja mengi yaliyosaidia kutoa mwangaza zaidi katika riwaya hizi.

## TANBIHI

1. J. Kitsao — Tamthilia alizowahi kuandika ni:- Mafarakano na michezo mingine - pamoja na Z. Zani, Uasi, Tazama Mbele, Malimwengu Ulimwenguni na Bibi Arusi

2. E. Hussein — Tamthilia alizowahi kuandika ni:- Kinjekatile, Mashetani, Arusi, Jogoo Kijijini wakati ukuta na Alikiona

3. E. Kezilahabi — Riwaya alizowahi kuandika ni:- Rosa Mistika, Dunia Uwanja wa Fujo, Kichwa Maji, Gamba la Nyoka, na Kichomi (ushairi)

4. S.A. Mohamed — Riwaya alizowahi kuandika ni:- Asali Chungu, Dunia Mti Mkavu, Utengano. Ushairi - Sikate Tamaa na Kina cha Maisha.

5. S. Robert — Riwaya alizowali kuandia ni:- Utubora Mkulima, Wasifu wa Siti bint Saad, Kusadikika, kufirika, Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini
Ushairi - Kielezo cha Fasihi, Koja la Lugha, Pambo la lugha na mapenzi bora

6. H. Arvon — Marxist Esthedics, Cornell Univ. Press, London 1973 uk. 24

7. Journal — Mulika No. 10 uk. 47

8. Magazine — The Weekly Review Sept. 20, 1985, uk. 27

9. Kama 6 hapo juu uk. 10

10. B. Lang and F. Williams — Marxism and Art, David Mckey Co. Press, NY 1972. uk. 10

11. Kama 10 hapo juu uk. 10

# SURA YA PILI

## KUMWANGALIA MKANGI

### 2.0 UTANGULIZI

Tunamwangalia Mkangi kama mwandishi chipukizi kwa kuchambua kazi zake mbili za fasihi - Ukiwa na Mafuta katika sura hii. Tunafanya hivyo kwa madhumuni ya kudhihirisha ufundi na ukuaji wake ama kurudi nyuma kwake katika utunzi.

Mkangi alianza kuandika riwaya yake ya kwanza ya Ukiwa mwaka wa 1970 na kuchapishwa mwaka wa 1975. Alianza kutunga Ukiwa bado akiwa mwanafunzi wa mwaka wa tatu katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Kama mwandishi wa Tanzania E. Kezilahabi alivyoanza Kichomi kwa kiingereza Mkangi naye alianza kuandika riwaya ya Ukiwa kwa Kiingereza lakini baada ya kushauriwa na marafiki zake akaiandika kwa Kiswahili kwa madhumuni ya kukikuza Kiswahili na pia ili watu wengi wa Afrika Mashariki waweze kukisoma[1]

Baada ya kuandika Ukiwa aliandika Mlo mswaada wa riwaya ambao haukuchapishwa kwa sababu za kisiasa. Baadaye akatunga hii riwaya ya Mafuta. Jambo hili linaeleza kwa nini kukawa na muda mrefu kati ya utolewaji wa riwaya hizi mbili. Hivi sasa yumo mbioni akiandika mswaada wa riwaya nyengine.

Kwa juhudi zake hizi tunamwona Mkangi kama mwandishi chipukizi aliyejawa na ari ya kupenda kujiendeleza katika uwanja wa fasihi sio kwa kutafuta jina bali kwa madhumuni ya kuwafunza wasomaji wake.

Tunamwangalia mtunzi huyu Mkangi kwanza katika Ukiwa halafu katika Mafuta kwa jumla na kutoa maoni kuhusu ufundi na uwezo wake katika utunzi. Tunafanya hivyo huku tukitilia maanani ya kwamba kubuni kazi ya fasihi si kitu rahisi. Hii ndiyo sababu si watu wote ni watunzi na si watunzi wote ni wazuri katika kazi zao. Wazo hili linatuelekeza katika ile dhana inayosema "utunzi, kama sanaa yoyote, ni kipawa na kipawa hiki chahitaji kupaliliwa ili kinawiri na kukua". Lengo letu kubwa ni kumwangalia Mkangi katika kazi zake hizi za fasihi kwa madhumuni ya kudhihirisha ufundi na uwezo wake katika uandishi, na kuamua ikiwa anaongeza nguvu na kukua katika uandishi wa fasihi ama anarudi nyuma.

Baada ya muhtasari wa riwaya zake tutaangalia uhodari wake wa kuchagua maudhui, uyakinifu wake katika kazi zake za fasihi na umahiri aliotuandalia katika kuzijenga riwaya zake. Hatimaye tutatoa maoni juu ya Mkangi na uandishi wake kama hitimisho.

.1.1. 'UKIWA'

Riwaya ya Ukiwa ilipewa mada hii kwa sababu ya ukiwa wa Matano ulioibuka kama matokeo yaliyomfika na kumwathiri mhusika huyu, Ukiwa huu ulikuja baada ya mapenzi yake na msichana Lila yalipokatika ghafla kabla ya kufika kilele cha ndoa kama Matano na aila yake walivyotarajia. Mada hii 'Ukiwa' inaoana na yaliyomo katika hadithi ya Ukiwa ambayo yenyewe inahusu mapenzi ya Matano na Lila ambao bado wamo masomoni. Hadithi hii inadhihirisha kiu ya mapenzi ya Matano ambayo ilichanua polepole na kupevushwa na visa vya mapenzi kati yake na Lila, lakini mwishowe kiu hii kamwe haikukimiwa na Lila, na matokeo yakawa ni ukiwa kwa Matano.

Hadithi yenyewe inaweza kugawanyika katika sehemu tatu muhimu. Sehemu kubwa na ya kwanza inaeleza namna Matano na Lila kama mvulana na msichana walivyoonana shuleni na baadaye kwa nyanyake Matano na kuanzisha uhusiano wao ambao ulikuwa chanzo cha mapenzi ya wawili hawa. Kuanza kwa urafiki wa Matano na Lila kulisaidiwa na nyanyake Matano. Baadaye tunaona urafiki wa Matano na Lila unashika moto na kuwasababisha wakutane mara kwa mara; mara nyingine katika

faragha na mara nyingine hadharani. Jambo hili liliwafanya wazoeane sana.

Sehemu ya pili vilevile inawahusu Matano na Lila ambao kwa taathira za elimu ya kizungu waliyoipata shuleni walijasiri wote wawili hasa Matano kujaribu kulegeza kamba za utamaduni alipokatikiwa kumwalika Lila kwao nyumbani kwa sherehe za krismas!. Jambo hili lilimtatiza Lila na kumwuliza Matano: "niende kwenu kama nani?" Kwa upande wa Matano naye baadaye aliingiwa na wasiwasi kwa sababu mila haikumruhusu kumleta Lila nyumbani kwa kina Matano. Msichana ambaye hakuposwa rasmi na mvulana hakuruhusiwa na mila kuenda nyumbani kwa wazazi wa mpenzi wake.

Lakini Matano alijitokeza kuvunja desturi hii kwa kumkaribisha na kumleta Lila nyumbani kwao. Hata hivyo Matano alikuwa na hofu kubwa kwa kitendo alichokifanya. Aliogopa sana vile babu yake na wazazi wake watakavyomkemea na hata kumtusi kwa kuvunja moja ya mila zao za jadi. Lakini kwa Sadfa Lila anakaribishwa vizuri nyumbani kwa kina Matano anapowasili. Lila anakaribishwa vyema kwa kumbatio kutoka kwa babu yake Matano ambaye alitazamiwa kuwa pingamizi kubwa. Jambo hili linampa Matano ushindi na majivuno.

Baada ya hapo mapenzi ya Matano na Lila yanashika moto na kufikia kilele cha kungojea ndoa tu ya wawili hawa huku wakiwa wameshaanza kupewa radhi na wazazi wa aila zote mbili. Lakini ni kweli walisema wahenga ya kwamba mtu hujua atokako bali hajui aendako. Mapenzi matamu ya Matano na Lila yalipofika kilele hiki cha kungojea ndoa yaligeuka ghafla na kuwa uchungu hasa kwa upande wa Matano ambaye kwa wakati huu alikuwa yu mtumwa wa mapenzi yake na Lila.

Kuharibika kwa mapenzi ya Matano na Lila ni chanzo cha sehemu ya tatu ya hadithi hii ya Ukiwa. Utengano wa Matano na Lila kimapenzi ulianza mara tu Lila alipopata safari ya kwenda Jijini kusomea kazi. Kufuatana na maelezo ya hadithi na falsafa za Matano na Vito kuhusu taathira za maisha ya Jijini kwa vijana hasa wasichana, yamkini Lila alitekwa na maisha ya anasa na upotovu Jijini kufikia kiwango cha kumtema Matano.

Lila alimpasulia Matano mbarika ya kumtema kama mpenzi wake katika moja ya likizo zake, ikawa Lila amezika mapenzi yaliyochanua, kunawiri na kuengwaengwa kwa karibu miaka mitano. Jambo hili lilimpa Matano Ukiwa - Ukiwa wa kuachwa macho makavu na mpenzi wake aliyempenda kwa pumzi zake zote na kwa moyo wake wote. Lakini basi -

yakimwagika hayazoleki. Isitoshe baada ya muda mfupi Matano aliongezewa ukiwa juu ya ukiwa na habari za kuaga dunia kwa Lila. Matano akaachwa na majonzi:

2.1.2 'MAFUTA'

Hadithi ya Mafuta imejengwa na visa vinavyosababishwa na kuongozwa na itikadi ya 'Mafuta' inayoshikiliwa na Wateule ambao ndio wenye nguvu za kisiasa na kiuchumi. Kwa mtu yeyote kuwa Mteule lazima awe na 'Mafuta' - yaani aamini itikadi ya 'Mafuta'. Wakati huo huo kuna visa vya upinzani vya wahusika wenye kuamini itikadi ya 'maji' ambavyo vinachochewa na itikadi ya 'Mafuta! Kwa sababu hii mada ya 'Mafuta' inawiana na maudhui ya hadithi hii kwa sababu hadithi nzima imejikita na kuzunguka katika itikadi hii ya 'Mafuta'.

Mafuta ni fumbo alilolifumba Mkangi na msomaji anatarajiwa kulifumbua. Riwaya yenyewe ina maudhui ya kisiasa na imeelezwa katika jumuiya ya jamii isiyokuwa katika ulimwengu bayana mithili ya riwaya ya Shaaban Robert, Kufikirika. Katika hadithi hii wahusika wamegawanyika katika matabaka mawili muhimu. La kwanza ni tabaka la Wateule ambao ni wahusika wenye nguvu za kiuchumi na za kisiasa. La pili ni tabaka la Matope ambalo ni tabaka la wahusika wanyonge wenye upungufu wa nguvu za

kiuchumi na za kisiasa. Tangu mwanzo wa hadithi hadi mwisho mna migogoro na migongano ya kitabaka kati ya matabaka haya mawili. Kiini cha migongano ya matabaka ya wahusika hawa ni tofauti zao za nguvu za kiuchumi na za kisiasa. Tofauti hizi zinaendelezwa pia katika itikadi za matabaka haya. Tabaka la wateule wana itikadi ya 'Mafuta' na alama yao ni'kitanda' ambacho mtu kukilalia lazima ujipake 'Mafuta' ambayo wanaamini ndiyo chanzo cha maisha. Kwa upande wa lile tabaka la wahusika wengine alama yao ni 'Matope' na itikadi yao ni 'maji' ambayo wanaamini ndiyo chanzo cha uhai.

Hadithi yenyewe inatolewa ikiwa mswaada wa mkulima Jali anayepatikana na janga la kusingiziwa wizi na mzee mwenye mkunazi wakati Jali anapookota kunazi moja tu kwa sababu ya njaa na kuionja. Kuitwa mwizi na mzee huyu kunasababisha Jali avamiwe na watu. Katika hali hii Jali analazimika kujisalimisha. Jali alitupa koti lake na kukimbia. Ni katika koti hili aliloliacha Jali ambamo mlikuwa na mswaada wa Mafuta ambao ulichukuliwa na watoto, kina Zuka na Kazamoyo. Watoto hawa na wenzao walizoea kucheza kamari chini ya mkunazi alipokuwa akiuza kunazi yule mzee mwenye mkunazi. Kwa hivyo tunaposoma hadithi ya Mafuta tunachukua mahali pa kina Zuka na Kazamoyo waliposoma mswaada wa Mafuta wa Jali.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

Kwa jumla anayeizungumzwa hadithi ya Mafuta ni Jali na anaanza na muhusika mkuu Mtue ambaye ana uwezo wa kuwa 'Mteule' lakini kwa hali ya ubinadamu na kuzinduka kwake anawahurumia wahusika wanaodhalilishwa walio katika tabaka la chini wajiitao' Matope', na wanaoishi katika vidimbwi vya matope, yaani wanaishi katika maeneo machafu. Hili Jambo la Mtue kuwaonea huruma wa kina Matope linamfanya achukuliwe kama mwasi wa tabaka la wateule. Lakini Mtue alisimama imara na kujitolea kuchunguza zaidi kiini cha uteule na hifadhi ya uteule wao pamoja na hali yao ya maisha. Kwa bahati anakutana na mhusika mwanamke aitwaye Ti. Ti ni mteule kizalia na anashikana urafiki na Mtue. Ti anamfunulia baadhi ya hali za wateule mpaka wanapokwenda mahakamani na kumkuta Matope mmoja wa kina 'Matope' - akishtakiwa kwa kumnajisi mama Fofi ambaye alikuwa karibu na kuwa mteule na kwenda kukilalia kitanda, kwa kumwosha kwa maji. Yaani Matope alishtakiwa kwa kusema ukweli kwa mama Fofi, kuwa 'Maji' ndiyo chanzo cha uhai wala si 'Mafuta'. Kosa hili lilichukuliwa kama kosa la uchochezi wa kutaka kuwazindua wahusika, na alihukumiwa kunyongwa. Mahakama yalipokuwa yanaendelea kisa kimoja kilimchongea Mtue kwa kumfanya acheke na Ti. Kosa hili lilimfanya Mtue naye afungwe jela na Ti

kusamehewa kwa sababu ni mteule. Karibu roba tatu ya riwaya inaeleza mambo ya mahakamani na kuhukumiwa kwa Matope.

Sehemu hii ya mahakamani inatudhihirishia wazi taathira za nguvu za kiuchumi katika jumuiya hii. Tunafunuliwa kupitia uzungumzi - nafsia wa Matope kwamba wakati Wateule wenye nguvu za kiuchumi na kisiasa wakula vinono na kunenepa kina Matope, ambao ni wanyonge, huwa wanataabika kwa njaa na mara nyingine kusababika kula makombo yaliyotupwa katika mapipa-jaa ambayo mengine huwa nje ya nyumba za Wateule. Jambo hili linaonekana wazi uk. 37 Matope anapotuarifu visa vyake vya kupigania riziki kwa kusema kimoyomoyo kwamba:

> "Udhoofu wa njaa hutupa wengi wetu ukali wa mama simba.....Masaza yenyewe ya kugombania basi! Mifupa yenye vinyama ambako uma hazikufika. Kingo za silesi ugali mkavu ambao hata kuku hushindwa kuudona. Wali uliovunda na vyapati vyakuchomeka. Kwa jumla, ni mabakia ambayo hata mbwa na paka hawahalisi kuyala. Ni makombo ya nmna hii ndiyo tuliyogombania sisi, panya na wengineo"

Hii ni taswira - kielelezo cha maisha ya kina Matope

walio wanyonge kisiasa na kiuchumi. Madhila, uonevu na njaa vilikuwa cheche zilizozusha harakati za ukombozi baada ya Mtue na Matope kuwekwa kizuizini.

Kutiwa ndani kwa Mtue na yeye Ti kusamehewa kulimzindua Ti na kumfanya ajiulize "haki iko wapi"? Kwa kujikinga na kulaumiza kuwa ndiye aliyesababisha Mtue kufungwa kwa sababu alimpeleka mahakamani na wakacheka wote, lakini yeye hakufungwa, ilimbidi atafute suluhisho. Suluhisho bora zaidi lililomjia akilini mwake ni kujinasua katika tabaka la wateule na itikadi zake. Ti alifanya hivyo hasa baada ya kutambua ukweli ulipo, kuwa 'Maji' ndiyo chanzo cha uhai wala si 'Mafuta'. Baada ya kukata kauli ya kujitoa katika tabaka la wateule ilimbidi asafiri katika vidimbwi vya Matope ajionee ukweli ulipo na pia kutafuta jamii na rafiki za Mtue ili awaeleze mambo yaliyompitikia Mtue.

Ti asafiri vidimbwini na kufika kwa jamaa na rafiki za Mtue na kuoshwa na 'Maji' - yaani kuzinduliwa zaidi baada ya mazungumzo mengi. Mwisho tabaka la kina 'Matope" wanaamua kujikomboa kutoka kwa tabaka la Wateule, wanajitayarisha na kwenda wapiga vita wateule. Kujikomboa huku kulienda sambamba kwa sadfa tu na kudadisiwa kwa Mtue na Dubwana na Dubwasha - viongozi vya wateule -

walipoamua kumwonyesha siri ya uteule kabla ya kumnyonga. Siri yenyewe ni kwamba uongo kwao ndio ukweli, na kuwa itikadi na alama zilizowaongoza na zilizowaunganisha Wateule na kuhifadhi maslahi yao zilikuwa ni za kipuzi, kama vile 'Mafuta' kuwa ni mikojo ya paka; na kulalia kitanda kuwa ni kutembea tu chini ya kitanda kilichotundikwa kwa kamba. Yote haya nitaswira ya kuonyesha huwa uongozi wa wateule haukuwa na msimamo na itikadi walizozishikilia hazikuwa na maana na kwamba uongozi wa namna hii hauna budi kupigwa vita kama vile tuonavyo "Matope' wanavyoamua kujikomboa kutoka kwa wateule.

## 2.2. UJENZI WA RIWAYA

Ni katika ujenzi wa riwaya ambapo tunauona ufundi na ujuzi wa mwandishi katika kuziumba kazi zake za kisanaa na kuziibusha na umbo tofauti na riwaya nyingine ijapo maudhui yaweza kuwa mamoja. Hili ndilo jambo ambalo lazifanya <u>ukiwa</u> na <u>mafuta</u> ingawa ni kazi za fasihi za mtunzi mmoja zina umbo tofauti kwa sababu zimeumbwa kwa mitindo tofauti. Hii inaoyesha ya kwamba Mkangi si mwandishi punguani wa mitindo katika ujenzi wa riwaya. Kwa jumla Mkangi anaonyesha uhuru na ujuzi wa kutumia baadhi ya mbinu mbalimbali za fasihi kama vile usimulizi, lugha na

wahusika katika kuzijenga riwaya zake.

MFULILIZO WA HADITHI

Katika Ukiwa mtindo alioutumia kuisumulia hadithi yake ni ule wa moja kwa moja ambapo visa na vitushi vya hadithi vimepangika kwa mfulilizo vikifuatana kimoja baada ya chengine kulingana na vilivyotukia. Huu ni mtindo wa kihadithi na umetumiwa sana na mtunzi mashuhuri Shaaban Robert katika riwaya zake kama vile Utubora Mkulima na Wasifu wa Siti binti Saad. Ijapo katika Mafuta pia ametumia mtindo huu wa usimulizi wa moja kwa moja na wenye uhaba wa mbinu rejeshi, iko tofauti kubwa kati ya mitindo ya kuzianzia na kuzimalizia riwaya hizi. Hadithi ya Ukiwa ina anza moja kwa moja tangu mwanzo hadi mwisho. Lakini katika Mafuta mna visa vinavyoitangulia hadithi ya 'Mafuta' hasa. Pia mna visa vinavyokuja baada ya hadithi ya 'Mafuta' hasa. Visa hivi vyote vinavyokuja kabla na baada ya hadithi ya 'Mafuta' hasa vinahusiana na hadithi yenyewe kwa namna mbili. Kwanza, visa vinavyokuja baada ya hadithi ya 'Mafuta' hasa ni visa vinavyoifunga riwaya ya Mafuta baada ya hadithi ya hadithi ya 'Mafuta' hasa kumalizika. Pili, visa vinavyokuja kabla ya hadithi ya 'Mafuta' hasa ni

kitayarisho na kiini cha hadithi ya 'Mafuta' hasa, na hadithi yenyewe ya 'Mafuta' ni kifafanuo cha kiini hiki. Ithibati ya kauli hii ni kwamba tunaona baada ya visa vinavyotayarisha hadithi ya 'Mafuta' vijana, Zuka na Kazamoyo, wanasoma hadithi yenyewe ya 'Mafuta', na baada ya kuimaliza kuisoma visa vinavyofuata hadithi hii ya 'Mafuta' vinaonyesha kuzinduka kwa vijana hawa Zuka na Kazamoyo na kutafuta maelezo zaidi kuhusu ukweli wa hadithi hiyo. Lakini baadaye wanaelewa na kujiuliza "Ni kwa kivipi ni yeye tu ndiye mwenye mkunazi?" na kuongeza "Inakuwaje ni yeye tu aruhusiye zitundwe, azipange mafungu, ayape bei yeye...? Ni yeye... kila kitu ni yeye! Na ukiangalia, tusio na mkunazi tu wengi!."

Tofauti nyingine inayojitokeza ni kuhusu wasimulizi wa hadithi za Ukiwa na Mafuta. Katika Ukiwa tunaona kwa urahisi ya kwamba mtunzi atuhadithia hadithi ya Ukiwa kupitia Matano ambaye ndiye mhusika mkuu. Lakini katika Mafuta tunaona mtunzi anavyojigawanya, kwa uhodari wa kima cha juu, katika nafsi mbili zinazochukua jukumu la kutusimulia hadithi ya Mafuta kwa jumla. Nafsi ya kwanza inajitokeza kama msimulizi wa visa vinavyokuja kabla na baada ya hadithi yenyewe ya "Mafuta". Nafsi ya pili ni nafsi ya ndani ya mtunzi inayojitokeza kama Jali aliye mtunzi na mwandishi msimulizi

wa mswaada wa hadithi ya "Mafuta" hasa. Kwa hivyo tunapochunguza ni nani msimulizi katika kazi zake za fasihi kuanzia na Ukiwa halafu Mafuta riwaya iliyoifuata Ukiwa, tunaona ule ustadi wa kima cha juu uliotumika katika Mafuta. Uhodari huu ndio unaomdhihirisha Mkangi kama mwandishi anayekua katika kipengeee hiki cha usimulizi kinacho changiza katika ujenzi wa riwaya nzima.

## MTINDO WA USIMULIZI

Fauka ya hayo mtindo wa kumfanya mhusika Matano kuwa msimulizi katika Ukiwa umedhihirisha dosari. Kwa mfano katika hadithi hatuonyeshwi visa vilivyompitikia Lila Jijini ambavyo vilimfanya Lila amteme Matano kama mpenzi na mchumba wake. Hii ni kwa sababu katika hadithi Matano ambaye ndiye msimulizi aweza kuwa pahali pamoja tu kwa wakati mmoja. Kwa hivyo Matano hakuweza kujua maisha ya wahusika wengine kikamilifu hasa maisha ya Lila huko Jijini kwa sababu Matano hakuweko Jijini. Iliyobaki ni Matano kutoa sababu kulingana na maelezo ya dhana na falsafa wanazozijua yeye na rafiki yake Vito kuhusu maisha ya Jijini - kuwa ni ya anasa kwa hivyo tubaini ya kwamba lazima Lila awe alitekwa na maisha ya Jijini, na kumkinika kupata mimba, na kuamua kumwacha Matano, na alipojaribu kuitoa mimba hiyo

dau likaenda mrama na Mungu akatwaa kiumbe chake, na kumwachia Matano ukiwa juu ya ukiwa. Kwa maoni yangu kuonyeshwa kwa visa vya maisha ya Lila Jijini kuna umuhimu mkubwa katika kuyaendeleza maudhui ya riwaya hii sawa na kuonyeshwa kwa visa vya kuanza na kukua kwa mapenzi yao. Hii yote ni kwa sababu Matano kama msimulizi hakuweza kuweko Jijini, na hii ni dosari ya kumfanya mhusika awe msimulizi.

Jambo jingine muhimu linalojitokeza katika usimulizi ni namna ya usimulizi. Katika riwaya zote mbili Ukiwa na Mafuta Mkangi anaonyesha ufundi uliosawa katika kutumia mchanganyiko wa mbinu za uzungumzi nafsia - unaotufunulia hisia za mhusika; mazungumzo ya wahusika na maelezo kutoka kwa msimulizi akieleza na kufafanua au kutilia mkazo mazungumzo ya wahusika na hadithi. Mfano wa uzungumzi nafsia katika Ukiwa ni pale Matano anapopata barua ya kifo cha Lila na kuwaza:-

> "Ulimwengu, wapi usawa wako?" niliwaza na kwa ghafla nikaanza kulia"[3]

Katika Mafuta pia uko mfano mahasusi wa uzungumzi nafsia kutoka kwa mhusika Matope. Alipopelekwa katika mahakama ya Wateule kabla ya kujitetea aliwaza:-

"Ningewaambia juu ya njaa na kiu
inisakatayo hivi wanaponikodolea
macho..... lakini wataweza kunielewa?
Niwaambie? Ningewaambia kisa hiki tu
kingewatosha (lakini).. ya nini
kuwaeleza chochote?"[4]

Mfano wa usimulizi wa kutumia mazungumzo ya wahusika na maelezo kutoka kwa msimulizi ni kama huu ufuatao kutoka kwa Ukiwa:

"Mbona hujampa mwenzako chochote"
bamdodo akaniuliza.
'Angalia! samahani nikamgeukia Lila
'Dada utakunywa chai ama soda?
'mmh!...' akawa na haja ya kusema ipi
'Sijasho hilo' akaeleza
'Soda basi ipi'?
'Yoyote'akajibu

Hapo nikaandaa vinywaji juu ya vimeza vitatu kila kimeza kilikuwa karibu na mtu mmoja, na juu ya kila kimeza kimoja bilauri ya soda"[5]

Kwa kuongeza, Mkangi anaonekana ni mtunzi anayependa kutumia hadithi katika usimulizi wa hadithi zake hasa katika kueleza dhana ama kisa fulani ambacho huwa wazi zaidi kikielezwa ama kushabihishwa na hadithi. Katika Ukiwa uk. 21,

anatoa hadithi ya mwarabu na ngamia ili kutueleza ombi la Matano kuhusu uchu wake kwa Lila. Vilevile katika uk. 76 anatumia hadithi ya marafiki wawili inayotolewa na mamake Matano ili kusisitiza na kutahadharisha wasomaji dhidi ya marafiki wa uongo. Mara nyingine pia Mkangi hutumia hadithi za kidini kama alivyofanya katika Ukiwa uk. 22 ambapo anatoa hadithi ya Mtakatifu Toma ili kueleza sababu zake za kutoamini wari wa Lila. Katika Mafuta moja ya hadithi alizozitumia ni ile ya mzee aliyekuwa kazi yake ni kutesa wafungwa na watoto wake saba waliotarajiwa kubuni sala kabla ya kula chakula. Dhamira ya kutoa hadithi hii ni kueleza ya kwamba msema kweli ndiye huadhibiwa, kwa sababu katika watoto hawa saba yule wa mwisho alibuni sala iliyoonyesha ukweli wa chakula kilikotoka, na mtoto huyu aliadhibiwa na wazazi wake.

Aidha Mkangi anaonyesha ni mtunzi anayezingatia matumizi ya lugha kulingana na muktadha. Mtindo huu ameutumia saha ili kutupa picha halisi ya visa pamoja na mazingira visa hivyo vinamotendeka. Kwa mfano katika Ukiwa Matano anapokuwa na mazungumzo na nyanyake ambapo kulingana na mila nyanyako ni bibiyo kwa hivyo mna uhuru wa kutaniana, basi lugha anayoitumia Matano ni ya utani kama tunavyoona hapa:-

"Hodi!" nilibisha huku nikiingia

"Ala! mume wangu ni wewe....

"Ndiyo... ndimi...shikamoo bibi"

"Marahaba bwana.. wajisikiaje?"

"Hofu kwako tu kisura nikaanza kumtania"[6]

Matano awapo na vijana wenzake vile vile-yeye na wenzake wanatumia lugha ya utaani. Kwa mfano Matano awapo na Ngilo wanazungumza hivi:-

"Nini kulala saa moja jioni? akamwuliza

"Niende wapi?" nikamjibu kinyonge

"Twende tukatembee"

"Sina hamu" nikamkatalia.

"Huna kwa sababu Lila amekupiga buti...

... hujui wasichana walivyo? Mtendee wema atakulipa kwa buti. Hawana shukrani"[7]

Lakini Matano awapo na mama mkwe anatumia lugha ya heshima, kama hapa:-

"Na dansi yenyewe iko wapi? aliniuliza

"Iko Sauni mama" nikamjibu kwa adabu

"... Ni ya pesa?"

"La mama ni ya harusi"[8]

Kwa sababu anatumia lugha ya mazungumzo basi hana budi kufupisha maneno. Hili ni jambo la kawaida. Kwa mfano kutumia "bibiye"[9] badala ya "bibi yake"

ama "mwanawe"[10] badala ya "mwana wake".

Mkangi amejidhihirisha, hasa katika Ukiwa kuwa ni mwandishi mwenye tabia ya kudokezea wasomaji hatima ya jambo muhimu analoanza kulielezea. Kwa mfano katika Ukiwa uk. 21, Matano mara tu kabla ya kutueleza ubembelezi wake kwa Lila ili akubaliwe aondoe uchu wake atangulia kutudokezea hatima ya kitendo hicho atakacho kukifanya kwa kutupa hadithi ya Mwarabu na ngamia na halafu anasema "Lakini mara hii Mwarabu hakumtimizia ngamia matakwa yake". Kwa fununu hii twajua tayari ya kwamba Matano sasa anajiingiza katika kumbembeleza Lila lakini hataambua chochote. Tena mara tu sehemu ya kuachana kwa Matano na Lila inapoanza tunaarifiwa hatima ya hadithi pale Matano anaposema:

> "…. kwamba (maisha yangu na Lila)
> yatabadilika na kuishia na kichuguu
> cha kaburi ni kitendawili, ambacho huenda
> pengine nami nikakifumbua nitakapositiriwa"[11]

Baada ya kusoma mawazo haya ya Matano tunajua mara moja ya kwamba hadithi hii itaishia na Matano kuachwa na Lila, na Lila naye aage dunia baadaye. Kwa hivyo ile ilhamu ya msomaji itarajiwayo kutokana na kujengwa kwa hadithi kwa mtindo wa kuficha visa na vijitokeze vyenyewe hadi kileleni na kuendeleza ile hamu ya kutaka kujua ni nini kitatokea baada ya

kisa hiki au hiki huwa inaondolewa, na msomaji hubaki anasoma tu ilimradi amalize kitabu. Iko mifano mingi ya namna hii katika Ukiwa. Ijapo mtindo huu wa usimulizi una uzuri wake - kwamba ndio tunajua hatima ni kifo kwa Lila, tutakalo ni kujua kitakuwa kifo cha aina gani. Lakini hata hivyo ubaya wa mtindo huu sana huuzidi uzuri wake. Kwa muktadha huu, uhaba wa hulka na mtindo huu katika Mafuta unaonyesha ukuaji wa mtunzi katika usimulizi.

Hata hivyo kuna jambo ambalo Mkangi amelionyesha kwa uzuri wa sawa katika riwaya zote ijapo katika Mafuta jambo hilo linaonyeshwa katika mafumbo. Jambo lenyewe ni kuhusu ufundi wa kueleza vitu na mandhari. Hueleza kwa ufundi na kwa kikamilifu. Kwa mifano katika Ukiwa tunaona maelezo haya:-

> "Kila jioni (nyanya) aligeuza ukumbi wa nyumba yake kuwa hoteli. Meza moja ndefu na ubao wa kulingana ndivyo vilikuwa vikalio vya hoteli hiyo mchwaramchwara. Wanunuzi walipakuliwa (wali) sahanini na kulia na vijiko ambavyo kila baada ya kutumiwa vilichovywa katika maji ya vuguvugu.... Taa kubwa la kopo lilitoa mwangaza... Taa lenyewe lilikunywa nusu lita ya mafuta kila siku" 12

Unaposoma ibara hii unapata picha halisi ya hoteli inayozungumziwa, na kujua ilikuwa ya hadhi ya namna gani, na ni watu wa aina gani waliokuwa wakienda katika hoteli hii.

Katika Mafuta pia tunaona maelezo haya ya mandhari:

> "Mahakama haya aliyoyaona, si kama haya tujuayo ... watu walikaa katika miduara Haijulikani nani hakimu, wakili mshtaki au mshtakiwa uingiapo. Kitu kilichoonekana wazi nikisehemu kidogo katikati ya mduara huu, safu ya kwanza, kukikaa wazee wa kike na wa kiume... Nyuso za hawa watu zilikuwa ngumu. Hakuna aliyekuwa akitabasamu au kuonekana kuwa na furaha"[13]

Unaposoma maelezo kama haya, ijapo ya kufumba, lakini unaiona ile picha ya mahakama ilivyo na tofauti yake kulingana na mahakama yetu tuliyozoea. Picha za vitu na za mandhari kama hizi tunazozipata kwa ufundi wa mwandishi wa kuelezea vitu zina saidia sana katika kuifuata hadithi na kuielewa licha na kuifanya hadithi iwe ya kuvutia zaidi.

Pia katika riwaya zote mbili Mkangi amejidhihirisha kama mwandishi mwenye hulka ya kukatisha mfulilizo wa visa katika sura moja na kipande

kilichobaki cha kisa hicho hicho kukifanya kianze sura inayofuata, pengine kwa kuchelea sura nyingine kuwa ndefu zaidi. Kwa mfano katika Ukiwa kisa cha mwisho cha sura ya pili kinaonekana kimekatwa na kipande kilichobaki kikaanza sura ya tatu kama ionekanavyo hapa:-

> ".... nilipotupa macho nje na kumwona Lila akiteremka basini... mzigo wangu wa wasiwasi ulinipotea mara tu nilipomwona.... Baada ya haya yote nilinyanyua hatua kwenda kumlaki"[14]
>
> (mwisho wa sura ya pili)
>
> (mwanzo wa sura ya tatu)
>
> "Hodi "- Hakumaliza kupiga hodi kwani nilikuwa nimeshafungua mlango.
> 'Huna haja' nikamkaliza
> 'Karibu ndani' nilimkaribisha"[15]

Vilevile katika Mafuta sehemu ya vitushi vinavyoeleza visa vya mahakamani ilikatwa katika sura ya nne na kipande kilichobakia kikaanza sura ya tano, kama tunavyoona hapa:-

> "Wakati huu vicheko viliishia midomoni kwani ni hapo lile njemba lilipojitokeza"[16]
>
> (mwisho wa sura ya nne)
>
> (mwanzo wa sura ya tano)
>
> "kuingia kwake (lile njemba) ghafla

kulikomesha kuteswa, kupigwa na
kudharauliwa kwa Matope"[17]

Ukatizi wa sura kama huu huwa unaathiri ule mtiririko wa visa na vitushi. Ni vyema kumaliza kisa kimoja ndipo kuanza sura nyingine aidha yenye uhusiano na kisa hicho au kilicho na kazi fulani katika hadithi hiyo.

## MATUMIZI YA LUGHA

Kwa upande wa lugha tunaona ya kwamba ijapo riwaya zote mbili zimeandikwa kwa lugha nyepesi na ya kueleweka, Mafuta imeizidi ukiwa katika lugha ya kitamathali. Jambo hili limeifanya riwaya ya Ukiwa ionekane kuwa ina lugha ya ufasaha na mtiririko mzuri wa mawazo kuliko riwaya ya Mafuta. Kulingana na fikira hizi wasomaji wengi aghlabu wanaipa umaarufu zaidi riwaya ya Ukiwa kuliko riwaya ya Mafuta.

Ni kweli kwamba Mafuta ina uhaba wa ufasaha wa lugha na wa mvuto na unati wa lugha ya kisanaa. Upungufu huu, kama Mkangi mwenyewe anavyodai[18] umesababishwa na uhaba wa maendelezi ya kibinafsi kuhusu lugha ya Kiswahili. Alipoandika Ukiwa alikuwa bado yuko Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam Tanzania na alikuwa anatilia mkazo kujifunza na kujiendeleza katika Kiswahili hasa kulingana na

uzito na umuhimu upewao Kiswahili katika nchi hiyo. Lakini baada ya hapo alishikilia utepe mwengine wa kusoma kwa chimbo zaidi somo linaloandikwa kwa Kiingereza la Elimu Jamii (Sociology) ambalo mpaka sasa ndilo analofundisha katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Kwa hivyo tofauti na waandishi wengine kama vile Jay Kitsao na E. Kezilahabi ambao huandika kazi zao za fasihi kwa Kiswahili na vilevile wanajishughulisha na maendelezi ya Kiswahili kibinafsi, kijamii na kielimu yeye huwa hashughulikii Kiswahili zaidi ya kukizungumza. Hii ndiyo sababu kwa nini lugha yake baada ya miaka kumi na minne (kutoka Ukiwa) inaonyesha upungufu wa ufasaha katika Mafuta.

Kuhusu matumizi ya mbinu za lugha ya kisanaa tunaona ya kwamba Mkangi ameonyesha kupanda ngazi kutoka Ukiwa hadi Mafuta hasa kwa upande wa kuzitumia mbinu hizo kwa kuifumba hadithi yake ya Mafuta. Mbinu za lugha alizozitumia sana katika riwaya zote mbili ni taswira, jazanda, majazi, tashbihi tashhisi, chuku na methali.

Katika Ukiwa kitendo kizima cha Matano na Vito cha kumuonya Lila kabla ya kwenda Jijini kinajitokeza kama taswira ya maisha ya Lila katika Jiji. Tunaona ama kupewa picha ya atakavyo yapitisha maisha yake Jijini na baadaye kuamua

kumuacha Matano. Jambo muhimu ni kwamba mbinu hii haikutumiwa kwa kifumbo zaidi kuliko katika riwaya ya Mafuta ambapo tunaona hadithi nzima kama taswira ya matendo ambayo yanaweza kuonekana ulimwenguni hasa katika nchi zinazoendelea. Mfano wa taswira nyingine iliyotumika kwa kufumba ni ile picha tupewayo katika Mafuta uk. 80 ya kuona nyuki akitafuta asali ukadhania yuko peke yake na ukamuua. Wengi huwa wako mzingani. Taswira hii imetolewa kama methali na inatuonyesha vile 'wateule' walivyowabana jela Mtue na Matope wakisahau kuwa wanawenziwao ambao kwa uchungu wa kubanwa kwa wenziwao wanaweza kujitokeza kwa ukali na kuwapiga vita 'wateule' kwa madhumuni ya kuwakomboa wenziwao na hao wenyewe kama tunavyoona baadaye karibu na mwisho wa hadithi.

Vilevile jazanda zilizotumiwa katika Ukiwa hazina ule uzito wa kufumba kuliko zile jazanda zilizotumiwa katika Mafuta. Moja ya jazanda inayojitokeza katika Ukiwa ni ile ya 'buyu' akimaanisha mimba. Hii ni jazanda ambayo kwa sababu inatumika sana mitaani inaanza kuwa na upungufu wa uzito wa kijazanda. Lakini katika Mafuta tunaona matumizi ya jazanda za hali ya juu ambazo zimeifumba hadithi ya Mafuta. Baadhi ya jazanda zilizotumika ni 'Mafuta' na 'Maji'. Jazanda hizi zimetumika kwa

namna mbili, kwanza, zinasimamia itikadi za jamii mbili tofauti katika ulimwengu huu wa kubuni wa riwaya hii. Jamii ya kwanza inaamini kuwa 'Mafuta' ndiyo asili ya uhai, na jamii ya pili inaamini kuwa 'Maji' ndiyo asili ya uhai. Pili, jazanda hizi zimetumika hadithini kwa sifa zao za kuwa Mafuta na maji yakiwekwa pamoja huwa hayachanganyiki bali mafuta huolea juu ya maji. Jazanda hii inaonyesha mambo mawili. Kwanza, waumini wa itikadi ya 'Mafuta' na waumini wa itikadi ya 'Maji' walikuwa daima wanautengano. Pili, waumini wa itikadi ya 'Mafuta' walikuwa wakitegemea waumini wa itikadi ya 'Maji' kwa maslahi yao. Yaani maslahi ya waumini wa itikadi ya 'Mafuta' yalikuwa yakibebwa na waumini wa itikadi ya 'Maji', kwa hivyo walikiishi kwa jasho la waumini wa itikadi ya 'Maji'.

Mbinu ya majazi imetumika sana katika riwaya ya Mafuta kuliko katika riwaya ya Ukiwa. Hii ni mbinu ambayo Mkangi aitumia kwa kupa baadhi ya wahusika wake majina ambayo yanaeleza hulka zao. Katika Ukiwa jina la Chawa linaeleza tabia aliyokuwa nayo ya kusaliti mapenzi ya rafiki yake Matano. Amepewa jina hilo kulingana na methali inayosema "kikulacho kinguoni mwako". Pia mhusika Kopo la Chooni naye amepewa jina hilo kama majazi ili kueleza uchafu wa tabia yake.

Katika Mafuta jina Matope ni majazi na linaeleza hali ya mhusika huyu kuwa ni duni, na pia ni mpungufu wa thamani mbele ya 'wateule' na aweza hata kutemewa mate. Majazi haya yanaendelezwa hata kwa wenzake wa akraba hiyo kwa sababu wote wanatumia 'Matope' kama alama yao wanayojitambulishia. Mtue ni jina alilopewa mhusika huyu kumaanisha kuwa alikuwa ni mhusika aliyetua na kumakinika. Tabia hizi zamfanya awe mvumilivu, mjasiri na mdadisi wa mambo. Jasho pia ni jina alilopewa mhusika huyu kuonyesha kuwa ni mtu wa bidii na hula jasho lake katika maisha.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

Tashihisi pia ni mbinu ambayo Mkangi ameitumia katika kuzijenga riwaya zake. Kwa mfano, katika ukiwa Matano anasema "..... nikaona siku za masomo haziendi bali za tambaa.[19] Hapa mwandishi amezipa siku uhai na kwamba hazikutembea haraka haraka bali zilitambaa polepole. Kwa sababu ya upweke aliokuwanao shule ni baada ya kuachana na Lila baada ya Krismasi.

Mtunzi pia hakuisahau mbinu ya Tashbihi ya kushabihisha kitu kimoja na chengine, Katika Ukiwa moja ya tashbihi zilizotumika ni "Basi lilienda mwendo wa kinyonga".[20] Hapa mwandishi anatupa picha ya jinsi basi hilo lilivyokuwa polepole kwa

kushabihisha mwendo wake na ule mwendo wa kinyonga. "Moyo ulichanuka kama ua la waridi"[21] ni moja ya tashbihi zilizochangiza katika kuifumba riwaya ya Mafuta. Hii ni tashbihi inayoeleza furaha ya Ti ya kuzinduka na kukaribishwa vizuri na akina Msati. Kwa hivyo mwandishi anaishabihisha furaha ya moyo wake na kuchanuka kwa ua la waridi, na ya kwamba moyo wake unaanza kupata nguvu mpya na furaha mpya katika mazingira ya ukweli halisi wa mambo yalivyo katika jumuiya ya ulimwengu huu wa kubuni.

Katika Ukiwa mbinu ya chuku pia haikutumika sana kuliko katika Mafuta. Katika Ukiwa chuku inaonekana pale Matano anapoeleza hali ya hoteli ya nyanyake anapoengeza na kusema "... pana taa la kopo... ambalo hunywa nusu lita ya mafuta". Hapa Mkangi anatia chumvi ili kusisitiza ukubwa wa taa hilo. Chuku hii pia yaweza kuchukuliwa kama tashhisi kwa sababu analipa uhai taa hili la kopo kusema "lilikunywa nusu lita ya mafuta." Katika Mafuta matumizi ya mbinu hii ya chuku kunaifanya riwaya hii ionekane kuwa imesumuliwa kimzahamzaha ijapo kwa makusudi na madhumuni fulani. Aghlabu mtu akikufanyia jambo la kuudhi lakini kimzahamzaha hutalichukulia. Baadhi ya chuku hizo ni pale mwandishi anapoeleza ukubwa wa tumbo la Dubwana -

asema alionekana kama "amebeba mimba nne". Pia anapoeleza kicheko cha Dubwana baadaye anasema "kicheko chake kilifanya kuta kutikisika". Isitoshe, Mkangi tunamuona akieleza chuki ya mama Fofi kwa chuku kweli anaposema "machozi yalimiminika kama yatokayo bombani".[23]

Mwisho kabisa tunamuona mwandishi ametumia mbinu ya methali na kidogo mbinu ya tasfida. Kuhusu methali, mfano wa kwanza kutoka kwa Ukiwa ni ule unaosema "mtu hujua atokako, hajui aendako.[24] Huu ni methali alioutumia kutuarifu kimbele. Kuwa msingi wa mapenzi walioujenga Matano na Lila huenda, ukaanguka, na wapenzi hao kutengana. "Kuishi kwingi, kuona mengi"[25] ni mfano wa pili wa methali aliyoitumia Mkangi katika Ukiwa. Ametumia methali huu ili kutuonyesha hekima ya wazee wanaoiegemea katika kupiga vita vijana dhidi ya mapinduzi ya utamaduni waliourithi kutoka kwa mababu na mababu zao. Katika Mafuta methali iliyotumiwa ni kama "weka mwizi ushike mwizi"[26] na "Akufukuzae hakwambii nenda."[27] Baadhi ya misemo ni kupiga moyo konde"[28] na kufunga kibobwe."

Ibara kama hizi "kuishia na kichunguu cha kaburi" na"... nitakapositiriwa" alizozitumia Mkangi katika Ukiwa uk. 87, na ibara ya "... kwao ulikuwa

mwisho wa ulimwengu," aliyoitumia katika Mafuta uk. 89 ni mifano ya mbinu ya tasfida aliyoitumia mwandishi. Hii ni mbinu ambayo mtunzi hutumia maelezo ya kitu au jambo badala ya kutumia neno baya au lenye uzito zaidi.

Ingawa Mkangi amezitumia mbinu hizi zote katika kuzijenga riwaya zake zote tunaona ya kwamba amezitumia kwa ufundi wa kufumba zaidi katika hadithi ya Mafuta kuliko katika hadithi ya Ukiwa. Jambo hili limeifanya Mafuta ionekane kuwa ni riwaya isiyoeleweka kwa urahisi na isiyo na lugha yenye mvuto na unati wa lugha ya kisanaa. Mtindo wa kufumba kama huu pia unapatikana katika Wema Hawajazaliwa, riwaya ya Ayi Kwei Armah; Ufundi wa Mkangi wa kutumia lugha ya kitamathali kwa kimafumbo zaidi katika riwaya yake ya pili ya Mafuta kuliko katika riwaya yake ya kwanza ya Ukiwa unadhihirisha ukuaji wa mwandishi huyu katika matumizi ya mbinu hizi za lugha ya fasihi.

UCHORAJI WA WAHUSIKA

Kuhusu wahusika Mkangi amewachora kulingana na dhamira yake kwa kuwapa umbo, hulka na kazi zinazochangiza katika kuzijenga hadithi zake kufikia kilele cha maudhui aliyoyadhamiria kuyawasilisha kwa wasomaji. Dhamira zake zimemfanya wahusika wengi awachore kama wahusika wa mraba mmoja. Kwa mfano Matano na Vito katika Ukiwa wamechorwa wazuri tu na Chawa amechorwa mbaya tu. Katika Mafuta Dubwana amechorwa mbaya tu tangu mwanzo wa hadithi mpaka mwisho wa hadithi. Wahusika wengine wamechorwa kuwa wana hali mbalimbali katika maisha kama ilivyo kawaida katika maisha ya binadamu. Katika Ukiwa Lila amechorwa mzuri na kuwa mbaya baadaye hasa kwa Matano na aila ya Matano. Katika Mafuta Mtue amechorwa mzuri kwa wa kina 'Matope' na mbaya kwa wateule.

Kwa upande wa tabia na kazi za wahusika katika hadithi tunamwona Mkangi kuwa ni mwandishi mwenye ufundi na uzingatiifu wa kazi za wahusika. Umahiri na uzingatiifu huu wa kazi za wahusika anauendeleza kutoka riwaya ya Ukiwa hadi riwaya ya Mafuta. Katika Ukiwa nyanyake Matano amechorwa kama mtani na mshenga wa Matano kwa Lila. Amepewa kazi ya kuwakutanisha Matano na Lila na kuwa pondo ya dau jipya la mapenzi ya Matano na Lila. Babake mdogo

Matano naye amechorwa rika moja na Matano ili Matano aone urahisi humleta Lila nyumbani kwa babake mdogo kwa faragha yao ya kwanza. Ngilo, amechorwa kijana mwenye tabia ya kuchangamka na amepewa kazi ya kumtoa nje Matano baada ya kutemwa macho makavu na Lila. Chawa, amepewa hulka ya rafiki wa uongo na kazi ya kusaliti mapenzi ya Matano na Lila, hali babu yake Matano, ambaye ni mwenye kuhifadhi utamaduni amepewa mawazo kimbele ya kulimka kiwakati ili asiweze kupinga jambo lolote bila ya kulipima kwanza kwa vile anajua maisha na nyakati vinabadilika. Amechorwa namna hii ili Lila akubaliwe nyumbani kwa kina Matano kwa urahisi kinyume na vilivyotarajiwa.

Katika Mafuta, Mtue amechorwa kuwa ni mhusika mwenye utu. Hulka hii inamfanya awaonee huruma wadhulumiwa. Ni huruma hii ambayo inamfanya aonekane kama mwasi na "wateule" kwa sababu Mtue anao uwezo wa kuwa mteule lakini anakataaa kujitambulisha nao kwa sababu ya athari za zinduko lililomgandama. Amepewa kazi, katika hadithi, ya kuwafunulia wasomaji hali ya 'wateule' na itikadi zao za kipuzi kama vile 'Mafuta' kuwa ni mikojo ya paka. Pia amepewa hulka ya kudadisi dadisi mambo kwa madhumuni ya kuwafunulia wasomaji kiini cha hali halisi ya jamii

anayoishi. Aidha Mtue kama mhusika mkuu amepewa tabia ya uvumilivu na ujasiri kwa madhumuni ya kuvumilia kuwa na "wateule" ili kutubainishia ya kwamba ukitaka kumpiga vita adui ni muhali umwelewe nje na ndani. Mambo haya yanajitokeza kwa sababu alimpiga vita Ti na akafaulu katika kazi yake ya kumzindua Ti.

Ti ni mhusika mwanamke ambaye kutoka mwanzo amechorwa kuwa ni mjasiri na amepewa sehemu ya kutubainishia ya kwamba 'wateule' pia huzinduka. Pia amepewa kazi ya kutuonyesha ya kwamba wanawake nao wanajukumu fulani katika harakati za ukombozi.

Msati ni mhusika aliyechorwa kama mzalendo anayeshikilia ule ukweli wa itikadi ya kusema ukweli. Kwa hivyo anapewa kazi ya kuwazindua na kuwaleta pamoja wazalendo katika mtaa wa Msokoteni na vitongoji vyake dhidi ya wadhalimu 'wateule'

Matope amechorwa mhusika mpole na mnyamavu na hohehahe asiye mbele wala nyuma kiuchumi, kwa mwandishi anavyomjua. Mhusika huyu amepewa kazi ya kuwakilisha na kudhihirisha hali ya tabaka la mafalahi wasio na nguvu za kiuchumi katika ulimwengu huu wa riwaya. Hukumu ya kifo ya Matope, na kutiwa ndani kwa Mtue na kusamehewa kwa Ti aliyefanya kosa sawa na Mtue na kusamehewa kwa sababu ya yeye ni 'mteule' inaonyesha ukosefu wa usawa na haki katika

jamii hii ya kubuni.

Kina Nyepi, Zaitu, Pakacha na Jasho wamechorwa kuwa ni wahusika wenye kujua ukweli ulipo, lakini kwa kuchelea fimbo ya 'wateule' huonelea jawabu zuri sana katika hali hii ni kutosema kabisa. Sululisho hili ndilo lililokuwa likifuatwa na wengi waliokuwa wakiishi katika vidimbwi vya Matope katika mtaa wa Msokoteni kabla ya zinduko lililowakumba.

Dubwasha na Dubwana ni wahusika waliopewa miili mikubwa na tabia za kikatili. Kama viongozi wa wateule wamepewa kazi ya maongozi ya kibavu katika jumuiya hii ya ulimwengu usiokuwa bayana.

Hata hivyo Mkangi ameonyesha dosari katika kuwaingiza hadithini baadhi ya wahusika na sehemu alizowapa wahusika hao. Kwa mfano mhusika kama Chawa ameingizwa katika hadithi ya Ukiwa kwa ghafla. Isitoshe visa vyake havionyeshwi bali tunaambiwa tu alikuwa rafiki wa Matano, na alisaliti mapenzi ya Matano na Lila. Hatuonyeshwi namna alivyoyasaliti mapenzi hayo. Hapewi mda wa kutosha hadithi. Pia Vito na Jison nao wanaingizwa mwisho mwishoni mwa hadithi katika wakati ambao dau la mapenzi la Matano na Lila linaelekea kwenda mrama. Hawa pia wanaingizwa ghafla mithili ya baada ya kukumbukwa na mtunzi. Msomaji huanza kujiuliza, ikiwa Vito

na Jison walikuwa marafiki wa Matano wa chanda na pete walikuwa wapi mapenzi ya Matano na Lila yalipoanza na kupevuka?

Kwa jumla wahusika wa riwaya zote mbili Ukiwa na Mafuta wamechorwa vizuri kulingana na dhamira ya mwandishi. Hata hivyo kuhusu uingizaji wa wahusika na kuwapa nafasi wahusika wenyewe watuonyesha vitendo vinavyotuelekeza katika maudhui riwaya ya Mafuta imeishida riwaya ya Ukiwa. Hii ni kwa sababu katika Ukiwa hasa karibu na mwisho wa hadithi tunaona sana maelezo ya vitendo kuliko vitendo vyenyewe. Kwa mfano, tunatanabahishwa kuwa Lila alikuwa na maisha ya anasa Jijini kwa falsafa za maisha ya Jijini, lakini hatuoni vile maisha ya anasa yalivyompitikia Lila. Pia tunaelezwa kuwa mapenzi ya Matano na Lila yalisalitiwa na Chawa, rafiki wa Matano lakini hatuonyeshwi kwa visa jinsi Chawa alivyoyasaliti mapenzi ya Lila na Matano.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

## 2.3 UTEUZI WA MAUDHUI

### MAUDHUI

Mkangi ni mwandishi ambaye ni hodari na mzingatiifu katika uteuzi wa maudhui. Katika kazi zake zote mbili Ukiwa na Mafuta amezungumza juu ya mambo ambayo yanawahusu na kuwapitikia watu

katika jamii. Aidha ni mwandishi anayedhihirisha kuguswa na hali na athari za maisha ya jumuiya za mijini dhidi ya mashambani, na zaidi maisha ya jumuiya za kibepari na kikabaila dhidi ya wanyonge katika jamii iwayo yoyote ile. Mambo haya yote yanadhihirika tunapoangalia aina ya maudhui aliyoyachagua Mkangi na kuyazungumzia katika riwaya zake.

Katika Ukiwa maudhui yanayojitokeza ni ya mapenzi na utamaduni. Mkangi anazungumza juu ya mapenzi ya vijana katika jamii. Kupendana kwa vijana ni jambo la kawaida na vijana kuachana na kuachiana ukiwa pia ni jambo linalopatikana katika jamii. Vile vile katika Ukiwa mtunzi anazungumza pia juu ya mapinduzi ya baadhi ya mila na desturi za Kiafrika. Hili pia ni jambo lililozagaa katika jamii zetu hasa jamii za nchi ambazo zinewahi kukumbwa na athari za tamaduni za Ulaya zilizoletwa kwa sababu ya uingiliano na wazungu kuhusu utawala na elimu ya Kizungu. Aghlabu tamaduni hizi za kigeni huwa zinapewa hadhi ya juu kuliko tamaduni za jadi. Kwa hivyo kuigiza tamaduni za kigeni hasa za kizungu huwa kunachukuliwa kuwa ni ustaarabu. Mpaka sasa wanasiasa bado wanapiga kelele hasa kwa vijana na kuwashauri kwamba utamaduni wetu ni vyema uhifadhiwe. Hata hivyo haimaanishi kuwa ni

tusiige tamaduni za kigeni kabisa, la hasha, bali ni tuchuje tamaduni hizo za kigeni na tuchukue zile tu ambazo zinatufaa na kutusaidia katika kuendeleza mbele mataifa yetu.

Katika Mafuta tunaona Mkangi amepiga hatua ya mbele zaidi na kuipa fasihi yake jukumu la kumlimsha msomaji juu ya athari za kiuchumi na kisiasa katika maisha ya jamii. Hii ni kwa sababu katika hadithi hii ya Mafuta tunaona maudhui makubwa na muhimu anayozungumzia Mkangi ni ya kisiasa yaliyofungamana na hali ya uchumi. Siasa na uchumi ni vitu viwili ambavyo vinaathiriana na kwenda sambamba kwa hivyo ni vigumu kuvitenganisha. Ni vitu ambavyo vinaathiri vipengee vyote vya maisha ya binadamu katika jamii ya jumuiya yoyote. Itikadi ya mwandishi katika maudhui haya ni "uongozi wa mabavu unaodumishwa na uongo kuufanya ndio ukweli hauna budi kuishia na mapinduzi". Ithibati ya itikadi hii ni kwamba katika hadithi uongozi dhalimu ulio mikononi mwa kikundi cha 'wateule' wanaoshikilia kuwa 'Mafuta' ndio chanzo cha uhai, na adui yao mkubwa akiwa 'Ukweli' mwisho wanapigwa vita na kundi linalojua ukweli ulipo kwa kuamini kuwa 'Maji' ndiyo chanzo cha uhai, na hadithi inaishia na kujikomboa kwa watu wa itikadi ya 'Maji'

kutoka mikononi mwa wateule kwa njia ya vita.

Ni katika maudhui na itikadi za mtunzi kama hizi ambamo tunamuona Mkangi kama mwandishi mtetezi wa wadhulumiwa, na pia mwandishi anayeandika kwa dhamira maalumu ya kututafsiria, ijapo kwa ufumbi, mambo yanayo wahusu na kuwapitikia binadamu katika jamii zao. Uteuzi wa maudhui kama haya kwa yakini unamfanya Mkangi aonekane kama mwandishi mwenye ubinadamu na anayezingatia maslahi ya wadhulumiwa kama misingi ya nadharia ya Kimarx inavyodokezea. Maudhui ya kisiasa kama haya ya Mafuta yanawagusa wasomaji hasa wale walioko katika nyingi ya nchi zinazoendelea ambako kunadhihirisho kubwa la matabaka ya watu wa kima cha juu na watu wa kima cha chini ambao aghlabu huwa ndio wengi. Kwa hivyo anayesoma Mafuta hakosi kujihusisha au kujitambulisha na tabaka mojawapo hasa lile la walio wengi - wanao shikilia itikadi ya 'Maji' - aidha aliunge mkono ama ajirudi anapostahili.

Fauka ya hayo uhodari na ukuaji wa kimaudhui wa Mkangi katika uteuzi wa maudhui hauishi hapo bali unaendelea kujitokeza hasa tunapoangalia vile maudhui makubwa aliyoyachagua katika Ukiwa na Mafuta yanavyofunika kama mwavuli maudhui mengi madogomadogo ambayo vilevile yanaihusu na kuiathiri

jamii kwa kiwango fulani. Kwa upande wa Ukiwa kuhusu mapenzi baadhi ya maudhui madogomadogo yanayojitokeza ni kwamba "utamaduni wa asili ndio unaotilia nguvu mapenzi kati ya vijana na kuwaongoza katika ndoa yenye radhi kutoka pande zote mbili za aila zinazohusika kama dondoo ifuatayo inavyotuthibitishia kauli hii ambapo Matano anasema:

> "tulikuwa vipenzi wa akraba zetu - wake
> na wangu - tulikuwa tumeshakubaliana
> maisha yetu ya mbeleni kuwa pamoja,
> na wazazi wetu pia walikuwa wameshakata
> shauri na kuanza kutupa radhi zao"[29]

Lakini utamaduni wa kisasa (Jijini) unaharibu mapenzi kama tunavyoona mapenzi ya Matano na Lila yalivyopwelewa mara tu Lila alipoenda Jijini kusomea kazi licha ya Matano na rafiki yake Vito kumonya Lila kabla ya safari yake kwamba:-

> "Maisha ya Jijini ni mapotevu sana.
> Tunakutahadharisha jinsi wasichana
> wengi walivyomezwa na maisha ya Jijini
> na mwisho wakajikuta wametapikwa na
> hawana maana tena. Wengi wajikuta ndani
> ya mitego waliyojiingiza huku wakiwaza
> 'I know what I am doing'.[30]

Katika Mafuta pia baadhi ya maudhui madogo-madogo yanayojitokeza ni "uongozi usiokuwa na msimamo daima haufanikiwi", mengine ni kwamba "nguvu za hali ya kiuchumi katika jamii ni nguzo muhimu sana katika uongozi na hadhi ya mtu katika jamii", Kauli hii inadhihirika zaidi tunapowaangalia "wateule" (wahusika wa tabaka la juu) walivyo; na hasa wanavyoishi kama walivyoelezwa hadithini kwa mifano:

> "Chumba kilikuwa cha vutia sana.
> Kilikuwa na madirisha mawili mapana...
> na urefu kuanzia sakafuni mpaka darini...
> vioo vilikuwa kila mahali..
> 'Je, vipi? usha amka? Ti akamuuliza Mtue
> huku akimpa chai.
> 'Sijui... kwani niko wapi?'
> 'Uzunguni' Ti akamjibu"[31]

Lakini kina yakhe wa kima cha chini kilichosababishwa na uhaba wao wa nguvu za kiuchumi walikuwa wa kiishi katika 'vidimbwi vya Matope vyenye kugasi mno'.

Maudhui madogomadogo haya yote katika Ukiwa na Mafuta, Mkangi ameyatumia kusaidia kuyajenga maudhui yake makubwa katika riwaya hizi ili afikie dhamira zake za kututafsiria na kutuelimisha juu

ya mambo aliyoyazungumzia.

Kulingana na misingi ya nadharia ya KiMarx tuliyochagua kama kigezo cha kuwangalilia Mkangi katika kazi zake za fasihi tunaona ya kwamba ijapo maudhui yote ya Ukiwa na Mafuta yanamulika maisha ya binadamu katika jamii lakini maudhui ya Mafuta yanauzito zaidi kuliko maudhui ya Ukiwa. Hii ni kwa sababu maudhui ya Mafuta yamejikita katika dhana muhimu za siasa na uchumi ambazo zinaathiri vipengee vyote vya maisha ya jamii - mapenzi na utamaduni vikiwemo. Kwa sababu hii tunaona ya kwamba Mkangi anaonyesha ukuaji katika uteuzi wa maudhui tukimwangalia kutoka riwaya yake ya kwanza ya Ukiwa kupitia riwaya yake ya pili ya Mafuta.

MAFUNZO

Kwa jumla maudhui yote aliyoyachagua Mkangi katika Ukiwa na Mafuta yamemuibusha kama mwandishi chipukizi mwenye kuzingatia mafunzo katika kazi zake za fasihi. Jambo hili linazipa kazi zake za fasihi jukumu na umuhimu wa kufunua na kuzindua wasomaji juu ya vipengee vya maisha anavyovizungumzia kama vile mapenzi na utamaduni. Jukumu la kufunza linasisitizwa sana katika nadharia ya fasihi ya ki Marx kama kazi moja wapo na muhimu ya fasihi.

Katika Ukiwa, kwanza Mkangi anawaonya vijana dhidi ya kumpenda mpenzi au mchumba kufikia kiwango cha kuwa mtumwa wa mapenzi hayo.[32]

Mantiki ya funzo hili ni kwamba mapenzi ni jambo la hiyari, na ni kama ua ambalo huchanua na kunawiri, likakomaa kisha baadaye hunyauka. Hili ni jambo la kweli kwa sababu hata wale waliopendana na kuoana muda fulani baada ya ndoa yao mapenzi hasa hufifia na kinachobakia ni kuvumiliana na kuheshimiana tu kwa mazoea. Kwa hivyo Mkangi anawatahadharisha vijana wapendane lakini pia kila mmoja aache nafasi ya uwezekano wa penzi hilo kukatika. Mtu akifanya hivyo hatadhurika mno kwa uzito wa ukiwa mara mpenzi wake anapohiyari kumtema wakati wowote. Funzo la pili kuhusu mapenzi na ndoa kwa vijana katika Ukiwa ni kwamba "usimwamini mchumba wako mpaka mfunge ndoa naye kwa sababu chochote chaweza kutokea na kukatiza kuoana kwenu. Aghlabu watu wengi katika mapenzi na ndoa huwa wanashikilia vitagaa viwili yaani kimoja kikikatika cha pili himsitiri. Tatu, Mkangi awatahadharisha vijana dhidi ya hadaa za ulimwengu ambazo hutatiza mapenzi ya wawili hasa wakitengwa na eneo kubwa na kuwa katika mazingira tofauti. Wazo hili linaambatana na ule msemo wa 'asiyekuwa

machoni (kwa mda mrefu) na moyoni hayumo'. Kwa muktadha huu tunafahamu vile Lila alivyo msahau Matano na alivyotekwa na maisha ya Jijini hadi kufikia kiwango cha kumtema aliyekuwa mpenzi na mchumba wake, Matano.

Kwa upande wa utamaduni, Mkangi anatutia moyo tujasiri kupiga vita baadhi ya mila na desturi zetu za Kiafrika kama vile kutoruhusiwa kumpeleka mpenzi wako nyumbani kabla ya wazazi wa aila zote mbili kujua kirasmi kwamba ni wapenzi na wachumba. Yako mafunzo mengi mengine katika Ukiwa ambayo yatategemea muktadha msomaji atakao uchukua.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY

Katika riwaya ya Mafuta vilevile mna mafunzo ambayo Mkangi kama mwandishi amedhamiria kuwapa wasomaji wake. Baadhi ya mafunzo hayo ni kwamba hali ya kinyonge na madhila ya patikanayo katika jamii si kudura ya Mwenyezi Mungu bali huwa na kiini chake katika jamii wala sio kutoka nje ya jamii hiyo. Kwa sababu hii, mtunzi atuonyesha ya kwamba madhila kama hayo yanaweza kuondoshwa kama vile watu wa 'Matope' walivyojikomboa kutoka kwa 'wateule' na dhuluma zao katika hadithi hii. Aidha anafunza na kuhimiza kwamba harakati za ukombozi kama hizi za hadithini za kuosha 'Mafuta' kwa 'Maji' nizakuendelea na pia si za kuachiwa wanaume peke

yao bali hata wanawake nao wana jukumu muhimu la kufanya katika shughuli kama hizi. Kauli hii inathibitishwa na pilka pilka za Ti na wanawake wengine kama Jasho katika harakati za kujikomboa kutoka kwa 'wateule' walioshikilia itikadi ya 'Mafuta'.

Tena katika Mafuta mwandishi afunza ya kwamba kuna mambo mawili muhimu kabla ya wanyonge - wenye 'Matope' - hawajajikomboa. La kwanza ni zinduko la wanaodhalilishwa na la pili ni umoja wao. Funzo hili linadhihirika tunapoangalia miondoko na visa vya wahusika kama vile Mtue na Msati katika hadithi. Mtue na Msati walizinduka kimbele na wakawa na wajibu wa kuwazindua sio waumini wa itikadi ya 'Maji' tu bali hata wale waumini wa itikadi ya 'Mafuta' kama vile Ti. Yamkini Msati aliifanya kazi hii ya kuwazindua wengine na kuwaleta pamoja kwa kisiri na kichinichini. Hii ni kwa sababu tunamuona Msati kwa mara ya kwanza katika ukurasa wa kwanza wa mwanzo ya hadithi akiwa na Mtue, kisha anatoweka na kutokea tena katika hadithi karibu na mwisho wa hadithi akiwa tayari ameshawazindua na kuwaunganisha wadhulumiwa, kina wa Matope, katika kundi kubwa la kutosha tayari kwenda wapiga vita wale wateule walio viongozi kwa madhumuni ya kujikomboa kutoka utawala wao. Maudhui na mafunzo

kama haya ya Mafuta yanafanana na ya tamthilia ya E. Hussein Kinjeketile inayotafsiri kisanaa vita vya majimaji nyakati za ukoloni wa Kijerumani.

Kuhusu mafunzo yaliyojitokeza katika riwaya hizi mbili Ukiwa na Mafuta kulingana na maudhui yaliyozungumziwa na mwandishi, tunaona ya kwamba ijapo yote yana umuhimu katika jamii lakini mafunzo ya Mafuta yana uzito zaidi kuliko mafunzo ya Ukiwa. Uzito huu unafuatana na uzito wa maudhui yanayozungumziwa katika riwaya hizi hasa tukitumia vigezo vya kazi ya fasihi (angalia sura uk. 7-11) kuambatana na misingi ya nadharia ya Ki marx. Ni kuzidi huku kwa mizani ya mafunzo ya Mafuta dhidi ya mizamii ya mafunzo ya Ukiwa ambako kunanipa ujasiri wa kuipa riwaya ya Mafuta sifa ya ukuaji kimaudhui na upevu wa kimawazo wa Mkangi kama mwandishi chipukizi wa fasihi riwaya za Kiswahili.

MISIMAMO NA FALSAFA ZA MWANDISHI

Kulingana na kazi zake hizi mbili Ukiwa na Mafuta Mkangi kama mwandishi - msomi na mwana Elimu Jamii anadhihirika kupenda kutoa misimamo na falsafa zake juu ya jambo analoliandika. Katika Ukiwa, kuhusu mapenzi Mkangi ashikilia kuwa

wawili wapendanao lazima wasameheane, wasaidiane na kuvumiliana katika miktadha mbalimbali kama vile katika maradhi, katika kukimiana mahitaji, na katika kupiga vita kutoka nje hasa kutoka kwa wafitini. Mkangi asema wapenzi hutimiza mambo haya kwa kupitia viwango vitatu:

1. Kiwango cha kwanza ni kile cha mwanzo wa mapenzi - umpendapo mpenzi wako kama alivyo - awe mchafu, mwizi, mwongo au katili. Huu ni wakati wa mapenzi yanapochanua, na wahenga husema ni wakati wa "kupenda chongo kuiita kengeza". Wapenzi wakifika kiwango hiki huingia kiwango cha pili.

2. Hiki ni kiwango ambacho hutokea ukinaifu katika kupendana na kuiita chongo chongo Wakati huu nyote ni mvumiliane mpaka kipindi hiki kipite na muingie kiwango cha tatu.

3. Katika kiwango hiki visa vya fitina na mafarakano wapenzi huvikiuka kwa ujasiri na hekima, na mapenzi hupevuka na kushika moto unaofikisha wapenzi hawa katika kilele cha ndoa.[33]

Katika falsafa hii tunamuona Mkangi atijitokeza kama mwandishi anayependekeza ndoa inayofuata baada ya wawili kuonana, kupendana, kufahamiana na kuzoeana kwa muda wa kutosha.

Mkangi pia anaona ya kwamba kutemwa ghafla na mpenzi umpendaye huleta mateso makubwa hasa kwa yule aliyetemwa. Hata hivyo ijapo anashikilia kuwa hakuna dawa ya mapenzi litokeapo jambo hili la kutemwa ghafla suluhisho bora zaidi ni kupiga moyo konde na kujikaza kisabuni kama mwanamume au kama mwanamke badala ya kukimbilia ulevi au kujiua.

Kwa upande wa utamaduni msimamo wake ni kwamba sheria nyingine za utamaduni wetu wa Kiafrika ni tuzibadilishe. Kwa sababu ya Lila kukubaliwa kwa sadfa nyumbani kwa kina Matano bila pingamizi yoyote kutoka kwa wazazi na wazee kinyume na ilivyotarajiwa inaonyesha kuwa Mkangi anatubainishia ya kwamba wazee sasa pia wanaanza kutambua mabadiliko ya nyakati, kwa hivyo wanakubali kushindwa ijapo mara nyingine kwa shingo upande. Kwa msimamo huu Mkangi anatia nguvu vijana hasa waliochochewa na elimu ya kizungu na tamaduni za kigeni kwamba hawana haja ya kuwaogopa zaidi wazazi wao katika kuvunja baadhi ya mila ambazo kwa wakati huu si mwafaka kuzifuata.

Katika Mafuta msimamo wake muhimu unaojitokeza ni ule wa "kusema ukweli hasa kuhusu hali halisi ya jamii". Msimamo huu ndio unaomwongoza katika Mafuta na kuchora hali halisi ya maisha katika jamii isiyokuwa ya ulimwengu bayana.

HITIMISHO

Kwa jumla Mkangi ni mwandishi anayedhihirisha ukuaji wa kimaudhui na kimawazo kama tulivyoona kupitia Ukiwa hadi Mafuta. Aidha ni mtunzi anayezingatia kuzungumza juu ya mambo ambayo yakini yanahusu au yanawapitikia binadamu katika jamii na kuhimiza mambadiliko. Kwa mfano, katika Ukiwa migongano ya mapenzi kati ya vijana wapendanao na mivutano kati ya vijana na wazee kuhusu utamaduni ni mambo ambayo yanawagusa wasomaji. Hii ni kwa sababu wako wengine ambao wamewahi kupitikiwa na visa vya ukiwa wa mapenzi aidha kwa kuachwa na wapenzi wao au kwa kufiliwa na wapenzi wao. Kwa upande wa utamaduni wako wasomaji wengine ambao wamewahi kupuuza baadhi ya mila na desturi za kabila lao kama vile kuchanjwa uso na kuvaa mavazi ya kitamaduni. Kuhusu mafuta wako pengine wasomaji waliowahi kupitikiwa na visa vya aidha kina Matope au wateule. Kwa hivyo wanaposoma riwaya hizi za Ukiwa na Mafuta huwa kwao zina ule mvuto wa

kuhusishwa katika hadithi anaouhisi msomaji

2.4. UYAKINIFU WA MKANGI KATIKA RIWAYA ZAKE

Katika riwaya zote mbili Ukiwa na Mafuta Mkangi amejishughulisha na mambo yanayopatikana katika jamii hasa za nchi zinazoendelea. Kwa mfano katika Ukiwa mgongano wa fikra na fikra katika mapenzi ya mvulana na msichana kama Matano na Lila, kisha baadaye kuachana si jambo geni katika jamii iliyohai. Aidha, mvutano wa kitamaduni wazee wakiwa upande mmoja na kushikilia kuendeleza tamaduni za jadi, na vijana wakiwa upande mwengine wakiathiriwa na elimu ya kizungu na tamaduni za kigeni na kushikilia kuleta mabadiliko katika utamaduni wa Kiafrika pia ni jambo ambalo sasa tumeshaanza kulizoea. Kwa hivyo mambo aliyoyazungumzia Mkangi ni ya kweli na yanakubalika. Tena kulingana na misingi ya nadharia ya Kimarx kuhusu kazi za fasihi pia tunamwona Mkangi kama mwandishi anayeandika kwa madhumuni maalum kama vile kumulika harakati za vijana katika kutafuta uhuru wa mapenzi dhidi ya pingu za utamaduni hasa kufuatana na mabadiliko ya wakati.

Swali la usawa pia limo katika Mafuta. Hadithi yote imejikita katika migongano ya wenye mali na wasio na mali. Katika hali hii wasio na mali

wanadhulumiwa, na kudhihirika kwa ukosefu wa haki katika jamii. Hili ndilo jambo ambalo linawachochea wadhulumiwa - kina Matope - na kutafuta sululisho la kujikomboa kwa kutumia nguvu zao ili wapate usawa katika jamii.

Kwa jumla Mkangi katika Mafuta kwa utumiaji wa taswira, jazanda na chuku za kufumba ametafsiri hali halisi ya maisha ya jamii hasa katika nchi zinazoendelea. Tafsiri hii licha ya kuwa inaaminika ina ukweli na jukumu la kuelimisha na kuasa jamii kisiasa. Kwa jumla ameshtumu zile hali halisi katika jamii ambazo zinawakirihi watu. Hii inaonyesha, kulingana na misingi ya nadharia ya Kimarx, ya kwamba Mkangi ni mwandishi ambaye anachukua maisha ya jamii kama malighafi ya kazi zake za fasihi na anachota taarifa zake kutokana na maisha hayo.

Kazi za fasihi za namna hii huathiri watu na pia hali ya jamii na kupendelea mabadiliko. Kwa mfano ukishtumu ndoa kati ya wazee na vijana basi huwa unapendekeza ndoa iliyojikita katika mapenzi.

Ukweli na uhalisi mwengine unaojitokeza katika riwaya ya Mafuta ni kwamba hakuna mtu hasa katika tabaka la 'wateuli' ambaye aweza kujisikia yu salama na ana furaha au yu huru kikweli ikiwa

usalama, uhuru na furaha yake vinategemea uoga na mateso ya wengine.

Kwa jumla kazi za Mkangi ni zao, muliko na tafsiri ya hali halisi ya jamii hasa za nchi zinazoendelea. Tafsiri hizi zina ukweli na ukubalifu na kama waandishi wengi wa fasihi Mkangi anadhihirisha fikira za ushindi kwa wanaojasiri kujikomboa kutokana na dhuluma ziwe za kisiasa ama za kitamaduni. Hata hivyo anatilia shaka ufanisi wa dhuluma za kimapenzi kwa sababu mapenzi ni jambo la hiyari.

## 2.5. HITIMISHO

Katika tungo hizi mbili Ukiwa na Mafuta Mkangi amedhihirika kuwa anaifahamu bahari anayoiabiri kwa ufundi unaokua hasa katika ujenzi wake wa riwaya na uteuzi wa maudhui kwa jumla. Mkangi vilevile ameonyesha kuwa ni mwandishi ambaye maisha yake yamebatilika, na thamani ya ubinafsi kwake si muhimu sana kuliko maisha mema ya watu. Kwa hivyo ni mwandishi aliyejitolea kuwaasa wasomaji wake juu ya vipengee vya maudhui yake ya mapenzi, siasa na utamaduni ijapo si wote watakaopata lengo la fasihi zake. Kwa muktadha huu ijapo yu chipukizi Mkangi si mwandishi anayeandika tu kwa

kutafuta jina na umashuhuri bali anaandika kwa madhumuni maalumu kama vile kutahadharisha vijana katika mapenzi, kuwazindua wazazi na wazee kuhusu mabadiliko ya wakati wa utamaduni, na pia kuwatetea wadhulumiwa. Dhamira hizi zote zatufanya tumuunganishe Mkangi na waandishi wenzake wa Kiafrika katika kufichua ukweli ulipo hata ule uliofichika katika mapenzi, siasa na utamaduni.

Hata hivyo wasomaji wengi wamemkaripia sana Mkangi kuhusu Mafuta kwamba ni riwaya ngumu wakiilinganisha na Ukiwa, na kuuliza: alikuwa akiwaandikia wasomi au wananchi wa kawaida? Kwa hakika Mafuta imeandikwa kwa ugumu, na ugumu wake unatokana na mafumbo yalotumiwa kuifumba riwaya hii. Hii ni kwa sababu ule wakati wa kuandika riwaya rahisi na kusomwa kwa starehe tu umepita. Sasa watu wamekua kimawazo na kiakili kwa hivyo tunahitaji riwaya zinazotufanya tutumie bongo zetu katika kutafsiri visa na mawazo ya mwandishi. Tena mtu akitanabahi nguvu za kijamii na kisiasa atabaini kiini cha ugumu wa riwaya hii.

Kuhusu ni nani aliyeandikiwa riwaya hii, yamkini mtunzi aliwaandikia wasomi kwa sababu wakulima aghlabu huwa hawana wasaa wa kusoma vitabu

vya fasihi. Jambo muhimu ni kukumbuka ya kwamba ukimfunza msomi umeelimisha jamii nzima kwa sababu ataeneza elimu aliyoipata na kuleta mabadiliko. Ndio, wakulima wanaweza kuleta mabadiliko lakini hutegemea uongozi wa wasomi kama kina Mtue na Msati.

Kukosa na kukosoana ni jambo la kawaida kwa binadamu. Kwa hivyo ijapo Mkangi ameonyesha dosari hapa na pale kama tulivyodokezea katika tasnifu hii dosari hizi zisitupofue kufikia kiwango cha kutoona mazuri mengi anayoyadhihirisha katika kazi zake za fasihi.

Kulingana na uchambuzi na uchanganuzi nilioufanya kuhusu Ukiwa na Mafuta kama kazi mbili za fasihi riwaya za Mkangi nimekatikiwa kuwa ni mtunzi chipukizi anayekua. Lakini kwa nini ni mwite mwandishi chipukizi? Mkangi ni mwandishi chipukizi kwa sababu ijapo alianza kitambo kuandika riwaya yake ya kwanza Ukiwa mwaka wa 1970 na kuichapisha mwaka 1975, na riwaya yake ya pili Mafuta akaichapisha mwaka 1985 bado aonekana kuwa yumo katika nyakati zake za mwanzo mwanzo wa utunzi kwa sababu ya idadi ya riwaya zake zilizoingia katika uwanja wa fasihi.

Ingawa Mkangi ni mwandishi chipukizi tunaona

kwa jumla, kupitia Ukiwa hadi Mafuta, ya kwamba kima chake cha kubuni kinaongezeka, hata yeye mwenyewe anaonyesha kufurahikia Mafuta zaidi kuliko Ukiwa kimawazo na kiufundi. Aghlabu mwandishi hupata ujuzi kutokana na mazoezi ya utunzi, na hili ni jambo ambalo Mkangi hakupungukiwa nalo. Kisha baadaye kwa ujuzi na umaarufu wake nafasi yake katika uwanja wa fasihi huhalalishwa na wasomaji wake kama afanyiwavyo E. Hussein katika uwanja wa tamthilia za Kiswahili. Mwandishi afikapo kiwango hiki wasomaji huweza kuona tofauti yake na watunzi chipukizi. Mkangi hivi sasa, akiwa na ari ya kuendelea, yumo katika barabara hii akijizatiti kusonga mbele tena kwa haraka.

## TANBIHI

1. Maoni haya niliyapata kutoka kwa mwandishi mwenyewe nilipozungumza naye kuhusu historia ya uandishi wake.
2. Mafuta uk. 92
3. Ukiwa uk. 102
4. Mafuta uk. 36-40
5. Ukiwa uk. 19
6. Kama 5 hapo juu. uk. 2
7. kama 5 hapo juu uk. 100
8. Kama 5 hapo juu uk. 27
9. Kama 5 hapo juu uk. 25
10. Kama 5 hapo juu uk. 28
11. Kama 5 hapo juu uk. 87
12. Kama 5 hapo juu uk 1
13. Mafuta uk. 21-22
14. Ukiwa uk. 16
15. Ukiwa uk. 17
16. Mafuta uk. 42
17. Mafuta uk. 42
18. Ithibati ya kauli hii ni mazungumzo niliyofanya na mtunzi mwenyewe
19. Ukiwa uk. 41
20. Ukiwa uk. 52
21. Mafuta uk. 65

22. *Ukiwa* uk. 1

23. *Mafuta* uk. 32

24. *Ukiwa* uk. 18

25. *Ukiwa* uk. 49

26. *Mafuta* uk. 15

27. *Mafuta* uk. 39

28. *Mafuta* uk. 54

29. *Ukiwa* uk. 1

30. *Ukiwa* uk. 81

31. *Mafuta* uk. 15

32. *Ukiwa* uk. 89

33. Ukiwa uk. 42

MAREJELEO

1. Ayi Kwei Armah, Wema Hawajazaliwa, Heinemann Edu. BKS, NRB, 1976

2. Henri Arvon, Marxist Esthetics, Cornell Uni. Press. London, 1973.

3. Hudson, W.H., An Introduction to the Study of Literature. Morrison & Gibb Ltd, London.

4. Jay Kitsao, Ph.D Thesis: An Investigation of Themes in Swahili Texts.

5. Katuu, D., Uchambuzi wa Vitabu vya Kiswahili, Bookwise Ltd, NRB, 1980.

6. Lang, B. & Williams, F. Marxism and Art. David Mckay Comp. Press. NY. 1972

7. Lee Baxandell, Radical Perspechives in the Arts, Penguin bks.

8. Mazrui, A., Mwongozo wa Mui Huwa Mwema na Uchambuzi wa Riwaya, Longman, NRB. 1981.

9. Mkangi, K.G.C. Mafuta, Heinamann Edu. Bks. NRB. 1984.

10. Mkangi, K.G.C. Ukiwa, Oxford Uni. Press. NRB, 1975.

11. Olsen, S.H. The Structure of Literary Understanging, Cambridge Un. Press, London, 1978

12. Robert, S., Kufikirika, Nelso E. Africa --

13. Robert, S. *Utubora Mkulima*, Nelson, E. Africa.---

14. Robert, S. *Wasifu wa Siti bint Saad*, Nelson E. Africa. 1978.

15. Said, A.M. Makala ya "Kupatana na Riwaya Zangu"

16. Sanchez, V.A. *Art and Society*. Merlin Press, London, 1973.

17. Wright, E., *The Critical Evaluation of African Literature* ----,----.

18. ----------- Jarida la Chuo Kikuu cha uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam, Vol. 43/1

19. ----------- Journal of the Institute of Swahili Research, Univ. of Dar-es-Salaam. Vol. 38/1

20. ----------- *Mulika* No. 10

21. ----------- *Mulika* No. 11

22. ----------- "The weekly Review", Sept. 20, 1985.

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY